Elimu ya Dini ya Kiislamu

Madrasa na Shule za Msingi

# Kitabu cha tatu



# Elimu ya Dini ya Kiislamu

Madrasa na Shule za Msingi

**Kitabu-III**

Islamic Propagation Center



Book3.indb 1 4/19/05 6:54:36 AM

Toleo la Pili 2006

Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.

©Hakimiliki 2006 IPC

Elimu ya Dini ya Kiislamu
Madrasa na Shule za Msingi
Kitabu cha Tatu

Wachapaji/Wasambazaji
Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.
Chapisho la Pili, 15, Desemba, 2006
Nakala 1000

Kimetayarishwa na Islamic Propagation Centre
P.O.BOX 55105, simu 022-22450069.

Usanifu wa kurasa na Michoro
Idd S. Kikong'ona
Katti-Ka-Batembo
Educomix Associates Ltd, Dar es Salaam.



Book3.indb 2 4/19/05 6:54:37 AM

## YALIYOMO


**SOMO LA KWANZA**

Hukumu za Usomaji Qur'an....1
- Idh-har....1
- Iq-labu....6
- Ikh-fai....6

Kusoma na kuhifadhi Quran....8
- Suurat twaariq....9
- Suuratul buruuj....10
- Suuratul Inshaqaq....12
- Suuratul Mutaffifina....14
- Suuratul Infitaar....17
- Suurat Takwiir....19
- Suuratu Abasa....22
- Suuratun Naaziaat....25
- Suuratun Nabai....29

**SOMO LA PILI**

Nguzo za imani....33

Dalili za kuwepo Allah (s.w) kutokana na Mwanaadamu....35
- Chanzo cha watu....35
- Lishe ya mtoto mchanga....37
- Kukua kwa mtoto....38
- Umbile la mwanaadamu na sura yake....39
- Mgawanyiko wa watu katika rangi, makabila na Mataifa....40
- Usingizi....41
- Kifo....42

**SOMO LA TATU**

Nguzo za Uislamu....45
- Kushahadia kwa vitendo....46
- Mnafiki....47
- Twahara....48
- Najisi....48
- Sharti za udhu....51
- Kutia udhu....51
- Kutoka na Udhu....53
- Sitara katika swala....53

Kuswali kwa wakati....54
Kuelekea Qibla....55
Nguzo za Swala....56
Baadhi ya Sunnah za Swala....57

**SOMO LA NNE**

Usafi....61
Unadhifu wa mwili....61
Unadhifu wa nguo....63
Unadhifu wa mazingira....64
Kumkumbuka Allah muda wote....68
Kumkumbuka Allah (s.w) wakati wa Ukimya....75

**SOMO LA TANO**

Uislamu kipindi cha Makka....77
Ujumbe wa Wahyi wa kwanza....77
Ujumbe wa Al-Muzammil na Al-Muddaththir....78
Kuanza kutangaza ujumbe....80
Kutangaza ujumbe kwa jamii mzima....81
Upinzani dhidi ya Uislamu....82
Mateso dhidi ya Mtume na Waislamu katika kipindi cha Makka....83
Waislamu watengwa ....87
Mtume (s.a.w) kwenda Taif kulingania Uislamu....88
Mafunzo kutokana na kuteswa Waislamu....89
Safari ya Miiraji....90
Mikataba ya Aqaba....93
Waislamu kuhamia Yathrib....94
Mtume(s.a.w) kuhamia Yathrib....94



Book3.indb 4 4/19/05 6:54:39 AM

## Neno la Awali

Shukrani zote njema anastahiki Allah (s.w). Rehema na Amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w) na wale wote wanaofuata njia yake.

Tunamshukuru Allah (s.w) kwa kutuwafikisha kutoa kitabu hiki cha Tatu kwa ajili ya watoto wetu wa Madrasa na Shule za msingi. Kitabu hiki ni katika mfululizo wa vitabu saba kwa ajili ya Madrasa zetu na shule za msingi.

Vitabu hivi vimeandaliwa kwa lengo la kuwawezesha watoto wa kiislamu kupata elimu ya msingi ya dini yao katika fani za Qur'an, Tawhid, fiqh, akhlad na tarekh.

Tunamuomba Allah atujaalie kulifikia lengo lililokusudiwa na atujaalie sisi na watoto wetu kuwa makhalifa wa Allah (s.w).

Wabillah Tawfiq

Mwalimu Mratibu
Islamic Propagation Centre



Book3.indb 5 4/19/05 6:54:40 AM

# Somo la 1. Qur'an

## KUSOMA NA TAFSIRI

**Hukumu za Usomaji Qur'an**
Kusoma Qur-an kwa kuzingatia hukumu zake ni jambo la lazima. Aallah (s.w) ametuamrisha:

وَرَتِّلِ ٱلْقُرْءَانَ تَرْتِيلًا

*… Na soma Qur-an vilivyo". (73:4)*

Kusoma Qur'an vilivyo ni kuisoma kwa mazingatio na kuitamka sawasawa ili ilete maana ile ile iliyokusudiwa.

Katika darasa hili la tatu tutajifunza hukumu za "***Nun Sakna***". Katika usomaji wa Qur-an, matamshi ya herufi zilizo mbele ya "***Nun Sakna***" ( نْ ) au "Tanwin"- Fatahtein ( ً ), kisratain ( ٍ ) na Dhummatain ( ٌ ) yatatoka kwa kuzingatia hukumu zifuatazo:

(1) Idh-har
(2) Id-gham
(3) Iqlab
(4) Ikhfai

**1. Idh-har**
Idh-har ni kudhihirisha au kuweka wazi. Kwa mnasaba wa usomaji, ni kuitamka herufi kama ilivyo au kuitoa katika uhalisi wake bila ya kuighunisha au kuikatisha. Kuna idh-hari za aina mbili: **idh-har halqiyi** ambayo matamko yake hutoka kooni na herufi zake ni sita na **Idh-har shafawiyyu** ambayo matamshi yake hutoka kwa kubana midomo miwili (shafatain), herufi zake ni ishirini na sita.

**(i)Herufi za Idh-har halqiyi**
Herufi za idh-har halqiyi zifuatao inabidi zidhihirishwe (na zitoke kooni) endapo nyuma yake yatakuwa na tanwin:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ا | ه | ع | ح | غ | خ |



Book3.indb 1 4/19/05 6:54:43 AM

**Mifano ya idh-har Halqiyi**

| HERUFI | TANWIN | NUN YENYE SAKINA | |
|---|---|---|---|
| ء | سِعٌ ءَلِيْمٌ | مَنْ ءَامَنَ | يَنْءَوْنَ |
| ع | رَسُوْلٌ أَمِيْنٌ | إِنْ هُوَا | يَنْحَوْنَ |
| ه | جُرُفٍ هَارٌ | مَنْ عَمِلَ | يَنْعِقُ |

**(ii) Herufi za idh-har Shafawiyyu**
Iwapo herufi yoyote ile mbali na **Bee** na **Mim** itafuatia baada ya Mim yenye sakna, basi Mim itatamkwa wazi na safi (itadhirishwa kwa kubana midomo miwili).

Mifano ya Idh-hari shafawiyyu (Idhi-hari ya midomo miwili):

Kwa **Alif**, **Hamza** na **Kaf**

وَلَا تُطِعْ مِنْهُمْ ءَاثِمًا، كَانُوْاهُمْ أَظْلَمَ،

فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ،

Kwa **Te** na **The**

أَمْثَالَهُمْ تَبْدِيلًا، أَلَمْ تَرَ كَيْفَفَعَلَ،

Kwa **ye**, **khe** na **waw**

أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ، هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ،

عَلَيْهِمْ وَلَاالضَّآلِّينَ،



Book3.indb 2 4/19/05 6:54:46 AM

Kwa **fei**, **dal**, na **dhal**

مَاسَلَكَكُمْ فِيْ سَقَرَ، لَكُمْ دِيْنُكُمْ،

مِنْهُمْ زُرِّيَّتَهُمْ،

Kwa **waw** na **re**

أَسْرَهُمْ وَإِذَاشِئْنَا، إِۦلَٰفِهِمْ رِحْلَةَ،

وَسَقٰهُمْ رَبُّهُمْ،

Kwa **shini** na **sini**

فَمَاتَنْفَعُهُمْ شَفٰعَةُالشَّفِعِينَ،

فَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا،

Kwa **twe** na **nuni**

وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا،أَلَمْ نَشْرَحْ،

Kwa **a'ini** na **ye**

إِذْهُمْ عَلَيْهَا قُعُوْدٌ، وَلَآ أَنْتُمْ عَابِدُوْنَ،

لَمْ يَكُنِ

## 2. Id-gham

Id-ghamu, katika lugha ya Kiarabu ni kuingiza kitu katika kitu. Katika istilahi ya Taj-wiid, ni kuchanganya herufi mbili na kuzitamka kama moja yenye Shadda. Id-ghamu imegawanyika katika mafungu mawili:

**(a)Id-ghamu zilizoko chini ya hukumu za *nunsakna* na *tanwin* nazo ni:**

(i)Id-ghamu pamoja na ghuna (Idghamu Naqis).
(ii)Id-ghamu bila ya ghuna (kaamil au taamma).

**(b)Id-ghamu ambazo haziko chini ya hukumu za *nunsakna* na *tanwin*:**

(i)Id-ghamu Al-Mutammathilayn.
(ii)Id-ghamu Al-Mutaqaaribayn.
(iii)Id-ghamu Al-Mutajaanisayn.

**(c) Id-ghamu chini ya hukumu za Nun sakna na Tanwin:**

Herufi zifuatazo iwapo zitakuja mbele ya ***nunsakna*** au ***Tanwin*** itabidi ziidighamishwe:

ل ر و ن م ي

(i) **Idghamu pamoja na ghunna** ni ile ambayo baada ya nunsakna na tanwin ikichanganywa na herufi za Id-ghamu hutokea sauti ya kughani. Ghunna ni sauti nzuri inayotoka katika mionzi ya pua. Herufi za id-gham pamoja na ghuna ni nne zifuatazo:

و ن م ي

Mifano ya idghamu pamoja na ghuna

| | TANWIN | NUN YENYE SAKINA |
|---|---|---|
| ي | وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَاعِمَةٌ | فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ |
| م | فِى كِتَابٍ مَّكْنُونٍ | عَمَّ يَتَسَآءَلُونَ |
| ن | عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ | عَنِ النَّبَإِ الْعَظِيمِ |



Book3.indb 4 4/19/05 6:54:50 AM

(ii) **Id-ghamu bila ya ghuna** ni ile ambayo baada ya ***nunsakna*** au ***tanwin*** ikikutana na herufi ya Idghamu, hutoa sauti moja bila ya ghunna. Herufi za id-ghamu bila ya ghunna ni mbili:

| | |
|---|---|
| ر | ل |

Mifano ya Id-ghamu bila ghunna:

| | TANWIN | NUN YENYE SAKINA |
|---|---|---|
| ر | لَعِبْرَةً لِأُولِي الْأَبْصَارِ | كَمَنْ لَا يَخْلُقُ |
| ل | يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ | ءَاتَيْنَاكَ مِنْ لَدُنَّا |

**(b) Id-ghamu zisizo chini ya hukumu za Nun Sakna na Tanwin:**

(i)**Id-ghamu al-Mutamaathilayn:** Hii hupatikana pale herufi yenye sakna inapokutana na herufi inayofanana. Mifano:

| | |
|---|---|
| إِضْرِبْ بِعَصَاكَ | ب |
| وَبَلْ لَا يَخَافُونَ | ل |
| وَقَدْ دَخَلُوا | د |

Mifano ifuatayo haidighamishwi ili isije kukosekana madda:

| | |
|---|---|
| الدُّنْيَا | بُنْيَانٌ |
| صِنْوَانٍ | قِنْوَانٌ |



Book3.indb 5 4/19/05 6:54:52 AM

(ii)**Id-ghamu al-Mutaqaaribaiyn:** Hii hupatikana pale herufi mbili zinazokurubiana kimatamshi na sifa, herufi iliyotangulia ikiwa na sakina. Mifano ya id-ghamu al-Mutaqaaribaiyn

| | |
|---|---|
| ث ذ | يَلْهَثْ ذٰلِكَ |
| ب م | يَابُنَيَّ ارْكَبْ مَعْنَا |
| ق ك | أَلَمْ نَخْلُقْكُمْ |

(iii) **Id-ghamu al-mutajaa nisain:** Hii hupatikana pale zinapokutana herufi mbili zilizo tofauti kisifa iliyotangulia ikiwa na sakna. Mifano ya id-ghamu al-mutajaa nisain:

| | |
|---|---|
| ط ت | لَئِنْ بَسَطْتَ |
| ت ط | وَكَفَرَتْطَّآ ئِفَةٌ |
| ت د | وَمَهَّدْتُ أَثْقَلَتْدَعَوَااللهَ |

**3.Iq-labu:**

Iq-labu maana yake katika lugha ya Kiarabu ni kukigeuza kitu kutoka kwenye asili yake. Katika Istilahi ya Taj-wiid, Iq-labu ni hukumu ya kugeuza matamshi ya ***NunSakna*** au ***Tanwin*** kuwa ***mimSakna*** iwapo herufi ya Iqlab itakuwa mbele ya nun-sakna au tanwin. Herufi ya Iq-labu ni moja, ***be*** .

| TANWIN | NUN YENYE SAKINA |
|---|---|
| لَنَسْفَعًابِالنَّاصِيَةِ | مِنْ بَعْدِ |
| خَيْرٌ بَصِيرًا | قَالَ يٰٓاٰدَمُ أَنْبِئْهُمْ |

**4. Ikh-fai:**

Ikh-fai ni kutamka herufi ambayo itakuwa kati ya Idh-hari na Id-ghamu kwa kuibakisha katika ghunna lakini bila ya Shadda. Kuna Ikhfai za aina mbili: Ikhfai Haqiqiyyu ambayo matamko yake hutoka kwenye mionzi ya pua (puani), na



Book3.indb 6 4/19/05 6:54:54 AM

Ikhfai shafawiyyu ambayo ina herufi mbili tu ***Mim*** na ***Bee*** ambazo kwa pamoja hutamkwa kwa kubana midomo miwili.

(i)Herufi za Ikh-fai haqiqiyyu:
Herufi ambazo zikiwa mbele ya ***NunSakna*** au ***Tanwin*** zitasomeka kwa hukumu ya Ikh-fai ni hizi kumi na tano zifuatazo:

| |
|---|
| ذ د ج ث ت |
| ض ص ش س ز |
| ك ق ف ظ ط |

Mifano ya Ikhfai haqiqiyyu:

| | TANWIN | NUN YENYE SAKINA |
|---|---|---|
| ث | مَآءًثَجَّاجًا خَيْرٌثَوَابًا خِلاَفٍ | مَنْشُوْرًا فَأَمَّا مَنْثَقُلَتْ |
| ج | حُبّاً جَمّاً فَصَبْرٌجَمِيْل | اَنجَينَاكُمْ مِنْجُوْعٍ |
| د | مَآءٍدَافِقٍ عَظِيْماً دَرَجٰتً | عِنْدَ مِنْدُوْنِ |
| ذ | عَزِيْزٌ ذُوانْتِقَام نَاراًذَاتَ | تُنْذِرُ مِنْ ذَالِكَ |
| ز | يَوْمَئِذٍزُرْقاً نَفْساًزَكِيَّةً | اَنْزَلْنٰهُ فَمَنْ زُحْزِحَ |
| س | بِقَوْمٍ سُوْءٍ شَفَاعَةً سَيِّئَةً | الإِنْسَانُ مِّنْ سِجِّيْلٍ |
| ش | نَفْسٍ شَيْئًا حِسَابًا شَدِيْداً | إِنْشَأَكُمْ فَمَنْ شَآءَ |
| ف | عَلَقَةً فَخَلَقَ | أَنْفُسِهِمْ مِنْ فِضَّةٍ |
| ق | عَبُوْساًقَمْطَرِيْراً شَيْءٍقَدِيْرٌ | يَنْقَلِبْ مِنْ قَبْلِكَ |



Book3.indb 7 4/19/05 6:54:57 AM

(ii)**Herufi za Ikhfai Shafawiyyu**: ***Mimsakna*** ikifuatiwa na ***Bee*** hukumu yake ni Ikhfau shafawiyyu. Mifano ya Ikhfai shafawiyyu:

| |
|---|
| قُلُوبُكُمْ بِهِ، يَأْتِيكُمْ بِهِ، مِنْهُمْ بَعْدَ ذَالِكَ، أَنْبِئْهُمْ بِأَسْمَآءِهِمْ |
| تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ، أُنَبِّئُكُمْ بِشَرٍّ، أَنْ يُصِيبَهُمْ بِبَعْضِ |
| لِأُنْذِرَكُمْ بِهِ، يَحْكُمْ بِ مَا تَ حُسُّونَهُمْ بِإِذْنِهِ |

**Kusoma na kuhifadhi Quran**
Mwanafunzi wa darasa la tatu adurusu mara kwa mara sura za Juzuu Amma alizokwisha hifadhi. Kisha aendelee kuhifadhi sura zifuatazo:-

Suratil Mursalaat hadi Surat Al-Jinn:

Katika kuhifadhi kwake azingatie hukumu za "Nun Sakna" na Tanwin". Pamoja na hivyo mwalimu amuelekeze mwanafunzi aweze kusoma kwa kuzingatia hukumu zote za usomaji.

**Tafsiri:**
Mwanafunzi wa darasa la tatu adurusu mara kwa mara tafsiri ya sura za Juzuu Amma alizozipitia darasa la pili. Kisha katika kipindi cha mwaka aweze kuhifadhi tafsiri za sura za Juzuu Ama zilizobakia, yaani kuanzia Atw-Twaariq hadi An-Nabaa.



Book3.indb 8 4/19/05 6:54:59 AM

# Suuratu twaariq

ina aya 17 | Makka

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

| | |
|---|---|
| 1. Naapa kwa mbingu na kwa hicho kijacho usiku | وَالسَّمَاءِ وَالطَّارِقِ ١ |
| 2. Na nini kitakachokujulisha kipi hicho kijacho usiku. | وَمَا أَدْرَاكَ مَا الطَّارِقُ ٢ |
| 3. Ni nyota inayong'ara sana! | النَّجْمُ الثَّاقِبُ ٣ |
| 4. Hakuna nafsi yoyote ila inayo mchungaji juu yake. | إِنْ كُلُّ نَفْسٍ لَمَّا عَلَيْهَا حَافِظٌ ٤ |
| 5. Hebu naajitazame mtu, ameumbwa kwa kitu gani? | فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ مِمَّ خُلِقَ ٥ |
| 6. Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa | خُلِقَ مِنْ مَاءٍ دَافِقٍ ٦ |
| 7. Yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo na kifua | يَخْرُجُ مِنْ بَيْنِ الصُّلْبِ وَالتَّرَائِبِ ٧ |
| 8. Kwa yakini Yeye ana uwezo wa kumrudisha | إِنَّهُ عَلَىٰ رَجْعِهِ لَقَادِرٌ ٨ |
| 9. Siku zitakapodhihirishwa siri. | يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ ٩ |
| 10. Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi. | فَمَا لَهُ مِنْ قُوَّةٍ وَلَا نَاصِرٍ ١٠ |
| 11. Naapa kwa mawingu yanayoleta mvua. | وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الرَّجْعِ ١١ |
| 12. Na kwa ardhi inayopasuka (ikatoa mimea). | وَالْأَرْضِ ذَاتِ الصَّدْعِ ١٢ |
| 13. Kuwa hii (Qur-an) ni kauli ipambanuayo haki. | إِنَّهُ لَقَوْلٌ فَصْلٌ ١٣ |



Book3.indb 9 4/19/05 6:55:33 AM

14. Wala si mzaha. — وَمَا هُوَ بِالْهَزْلِ ﴿١٤﴾

15. Hakika wao wanafanya hila — إِنَّهُمْ يَكِيدُونَ كَيْدًا ﴿١٥﴾

16. Na mimi nazipindulia mbali hila zao. — وَأَكِيدُ كَيْدًا ﴿١٦﴾

17. Basi wape makafiri muda, wape muda kidogo (wataona sasa hivi). — فَمَهِّلِ الْكَافِرِينَ أَمْهِلْهُمْ رُوَيْدًا ﴿١٧﴾

## Suuratul Buruuj

*ina aya 22* — *Makka*

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

1. Naapa kwa mbingu zenye Buruji (nyota) — وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْبُرُوجِ ﴿١﴾
2. Na kwa siku iliyoahidiwa (kuwa itafika, nayo ni siku ya Kiama) — وَالْيَوْمِ الْمَوْعُودِ ﴿٢﴾
3. Na Mwenye kushuhudia na kishuhudiwacho — وَشَاهِدٍ وَمَشْهُودٍ ﴿٣﴾
4. (Kuwa) wameangamizwa watu waliowaadhibu Waislamu katika mahandaki. — قُتِلَ أَصْحَابُ الْأُخْدُودِ ﴿٤﴾
5. Yenye Moto wenye kuni (nyingi) — النَّارِ ذَاتِ الْوَقُودِ ﴿٥﴾
6. Walipokuwa wamekaa hapo — إِذْ هُمْ عَلَيْهَا قُعُودٌ ﴿٦﴾
7. (wakati walipokuwa) wanatazama yale wanayowafanyia hao Waislamu (walipokuwa wakiwaadhibu). — وَهُمْ عَلَىٰ مَا يَفْعَلُونَ بِالْمُؤْمِنِينَ شُهُودٌ ﴿٧﴾



Book3.indb 10 4/19/05 6:55:48 AM

8. Nao hawajaona baya lolote kwao ila kumuamini Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda, Mwenye kusifiwa

وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَنْ يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ
الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٨﴾

9. Ambaye ni Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushuhudia kila kitu.

الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ
وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٩﴾

10. Hakika wote waliowaadhibu Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, kisha wasitubie basi watapata adhabu ya Jahannamu na watapata adhabu ya kuungua (barabara)

إِنَّ الَّذِينَ فَتَنُوا الْمُؤْمِنِينَ وَ
الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَتُوبُوا فَلَهُمْ عَذَابُ
جَهَنَّمَ وَلَهُمْ عَذَابُ الْحَرِيقِ ﴿١٠﴾

11. Hakika wote walioamini na kutenda vitendo vizuri bila shaka watapata Mabustani yenye mito ipatayo mbele yake. Huku ndiko kufuzu kukubwa.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ
ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْكَبِيرُ ﴿١١﴾

12. Hakika kutesa kwa Mola wako ni kukali (sana).

إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١٢﴾

13. Yeye ndiye aliyeanzisha (viumbe) na Ndiye atakayawarejeza.

إِنَّهُ هُوَ يُبْدِئُ وَيُعِيدُ ﴿١٣﴾

14. Naye ni mwingi wa msamaha Mpenda (waja wake)

وَهُوَ الْغَفُورُ الْوَدُودُ ﴿١٤﴾

15. Mwenye kiti cha enzi kitukufu

ذُو الْعَرْشِ الْمَجِيدُ ﴿١٥﴾

16. Mwingi wa kutenda alipendalo.

فَعَّالٌ لِمَا يُرِيدُ ﴿١٦﴾

17. Je, zimekuwasilia habari za majeshi ya makafiri?

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْجُنُودِ ﴿١٧﴾

18. Firauni na Thamudi.

فِرْعَوْنَ وَثَمُودَ ﴿١٨﴾



Book3.indb 11 4/19/05 6:56:14 AM

19. Lakini waliokufuru wamo katika kukadhibisha tu.

بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي تَكْذِيبٍ ﴿١٩﴾

20. Na Mwenyezi Mungu amewazunguka kote kote (hawawezi kuikimbia adhabu Yake).

وَاللَّهُ مِن وَرَائِهِم مُّحِيطٌ ﴿٢٠﴾

21. Bali hii ni Qur-an tukufu. (Iliyotolewa)

بَلْ هُوَ قُرْآنٌ مَّجِيدٌ ﴿٢١﴾

22. Katika huo ubao uliohifadhiwa.

فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٢٢﴾

## *ina aya 22* — Suuratul Inshaqaq — *Makka*

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

@

1. Mbingu zitakapopasuka

إِذَا السَّمَاءُ انشَقَّتْ ﴿١﴾

2. Na zitakapokinga sikio kwa Mola wake (kusikiliza amri); na zimepasiwa (na kusikiliza).

وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ﴿٢﴾

3. Na ardhi itakapotandazwa (itakaponyoshwa)

وَإِذَا الْأَرْضُ مُدَّتْ ﴿٣﴾

4. Na kuvitoa vilivyokuwa ndani yake, ikawa tupu.

وَأَلْقَتْ مَا فِيهَا وَتَخَلَّتْ ﴿٤﴾

5. Na ikakinga shikio kwa Mola wake; na imepasiwa (na kusikiza).

وَأَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ ﴿٥﴾

6. Ewe mtu! Hakika wewe unajikusurukusuru (katika kufanya mambo yako) mpaka (siku utakapokutana na) Mola wako; basi (amali zako hizo) utazikuta.

يَا أَيُّهَا الْإِنسَانُ إِنَّكَ كَادِحٌ إِلَىٰ رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلَاقِيهِ ﴿٦﴾

| | |
|---|---|
| 7. Ama atakayapewa daftari lake katika mkono wake wa kulia. | فَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَٰبَهُۥ بِيَمِينِهِۦ ۝٧ |
| 8. Basi yeye atahisabiwa hisabu nyepesi. | فَسَوْفَ يُحَاسَبُ حِسَابًا يَسِيرًا ۝٨ |
| 9. Na atarudi kwa watu wake (Peponi), na hali ya kuwa ni mwenye furaha. | وَيَنقَلِبُ إِلَىٰٓ أَهْلِهِۦ مَسْرُورًا ۝٩ |
| 10. Lakini atakayapewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake. | وَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَٰبَهُۥ وَرَآءَ ظَهْرِهِۦ ۝١٠ |
| 11. Basi yeye atayaita mauti (yamjie; ili afe apumzike, wala hayatamjia). | فَسَوْفَ يَدْعُوا۟ ثُبُورًا ۝١١ |
| 12. Na ataingia Motoni. | وَيَصْلَىٰ سَعِيرًا ۝١٢ |
| 13. Maana alikuwa na furaha (za maasia) pamoja na watu wake | إِنَّهُۥ كَانَ فِيٓ أَهْلِهِۦ مَسْرُورًا ۝١٣ |
| 14. (Na) alidhani kuwa hatarejea (kwa Mwenyezi Mungu). | إِنَّهُۥ ظَنَّ أَن لَّن يَحُورَ ۝١٤ |
| 15. Kwa nini (asirejee)? Mola wake alikuwa akimuona; (kwa hivyo atamlipa kwa kila aliyoyafanya). | بَلَىٰٓ إِنَّ رَبَّهُۥ كَانَ بِهِۦ بَصِيرًا ۝١٥ |
| 16. Basi ninaapa kwa wekundu (wa jua lichwapo). | فَلَآ أُقْسِمُ بِٱلشَّفَقِ ۝١٦ |
| 17. Na kwa usiku na unavyovikusanya. | وَٱلَّيْلِ وَمَا وَسَقَ ۝١٧ |
| 18. Na kwa mwezi unapokamilika. | وَٱلْقَمَرِ إِذَا ٱتَّسَقَ ۝١٨ |
| 19. Mtakutana na hali baada ya hali. | لَتَرْكَبُنَّ طَبَقًا عَن طَبَقٍ ۝١٩ |



Book3.indb 13 4/19/05 6:56:49 AM

| | |
|---|---|
| 20. Basi wana nini hawaamini? | فَمَا لَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٠﴾ |
| 21. Na wanaposomewa Qur-an hawanyenyekei? | وَإِذَا قُرِئَ عَلَيْهِمُ الْقُرْآنُ لَا يَسْجُدُونَ ﴿٢١﴾ |
| 22. Lakini wote waliokufuru wanakadhibisha (tu). | بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا يُكَذِّبُونَ ﴿٢٢﴾ |
| 23. Na Mwenyezi Mungu anajua wanayoyakusanya. | وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُوعُونَ ﴿٢٣﴾ |
| 24. Basi wabashirie adhabu iumizayo. | فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢٤﴾ |
| 25. Isipokuwa wote walioamini na kutenda vitendo vizuri; hao watakuwa na ujira usiokoma (usiomalizika). | إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٢٥﴾ |

## ina aya 36 — Suuratul Mutaffifiina — Makka

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

| | |
|---|---|
| 1. Maangamizo yatawathubutukia wapunjao (wenziwao) | وَيْلٌ لِلْمُطَفِّفِينَ ﴿١﴾ |
| 2. Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili. | الَّذِينَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ ﴿٢﴾ |
| 3. Lakini wanapowapimia (watu) kwa vibaba au mizani wao hupunguza. | وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٣﴾ |
| 4. Je! Wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa? | أَلَا يَظُنُّ أُولَٰئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ ﴿٤﴾ |
| 5. Katika Siku iliyo kuu. | لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٥﴾ |
| 6. Siku watakaposimama watu mbele ya Mola wa walimwengu? | يَوْمَ يَقُومُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦﴾ |



Book3.indb 14 4/19/05 6:57:09 AM

| | |
|---|---|
| 7. Sivyo hivyo (mnavyofanya)! Kwa hakika maandishi (ya amali) za waovu yamo katika Sijjin - | كَلَّآ إِنَّ كِتَٰبَ ٱلْفُجَّارِ لَفِى سِجِّينٍ ۝٧ |
| 8. Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ujue hiyo) sijjin ni kitu gani! | وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا سِجِّينٌ ۝٨ |
| 9. Ni daftari lililoandikwa (ndani yake amali za watu wabaya). | كِتَٰبٌ مَّرْقُومٌ ۝٩ |
| 10.Adhabu kali siku hiyo itawathubutukia wanaokadhibisha! | وَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ۝١٠ |
| 11.Ambao wanaikadhibisha Siku ya Malipo. | ٱلَّذِينَ يُكَذِّبُونَ بِيَوْمِ ٱلدِّينِ ۝١١ |
| 12.Wala haikadhibishi ila kila mwenye kuruka mipaka, mwenye dhambi. | وَمَا يُكَذِّبُ بِهِۦٓ إِلَّا كُلُّ مُعْتَدٍ أَثِيمٍ ۝١٢ |
| 13.Anaposomewa Aya Zetu husema: "Ni visa vya watu wa kale." | إِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِ ءَايَٰتُنَا قَالَ أَسَٰطِيرُ ٱلْأَوَّلِينَ ۝١٣ |
| 14.Sivyo hivyo! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao (maovu) waliyokuwa wakiyachuma. | كَلَّا ۖ بَلْ ۜ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا۟ يَكْسِبُونَ ۝١٤ |
| 15.Sivyo hivyo! Hakika watazuiliwa, siku hiyo na (neema za) Mola wao. | كَلَّآ إِنَّهُمْ عَن رَّبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّمَحْجُوبُونَ ۝١٥ |
| 16.Kisha wataingia katika Moto (uwakao). | ثُمَّ إِنَّهُمْ لَصَالُوا۟ ٱلْجَحِيمِ ۝١٦ |
| 17.Kisha waambiwe: "Haya ndiyo mliyokuwa mkiyakadhibisha". | ثُمَّ يُقَالُ هَٰذَا ٱلَّذِى كُنتُم بِهِۦ تُكَذِّبُونَ ۝١٧ |



Book3.indb 15 4/19/05 6:57:27 AM

18.Sivyo hivyo (mnavyofanya) Hakika Maandishi ya (amali za) watu wema yamo katika (daftari linaloitwa) Illiyyin.

كَلَّآ إِنَّ كِتَٰبَ ٱلْأَبْرَارِ لَفِى عِلِّيِّينَ ﴿١٨﴾

19.Na ni jambo gani litakalokujulisha hata uijue hiyo (illiyin) ni kitu gani -

وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا عِلِّيُّونَ ﴿١٩﴾

20.(Hilo) ni daftari ambalo zinaandikwa humo (amali za watu wazuri).

كِتَٰبٌ مَّرْقُومٌ ﴿٢٠﴾

21.Wanaliona wote waliokaribishwa (na Mwenyezi Mungu).

يَشْهَدُهُ ٱلْمُقَرَّبُونَ ﴿٢١﴾

22.Kwa hakika wafanyao wema watakuwa neemani.

إِنَّ ٱلْأَبْرَارَ لَفِى نَعِيمٍ ﴿٢٢﴾

23.Wakae juu ya viti vya fakhari waitazame (starehe zao).

عَلَى ٱلْأَرَآئِكِ يَنظُرُونَ ﴿٢٣﴾

24.Utaona alama za neema katika nyuso zao.

تَعْرِفُ فِى وُجُوهِهِمْ نَضْرَةَ ٱلنَّعِيمِ ﴿٢٤﴾

25.Watanyweshwa vinywaji (vizuri) vilivyofungwa (kwa vizibo madhubuti).

يُسْقَوْنَ مِن رَّحِيقٍ مَّخْتُومٍ ﴿٢٥﴾

26.Mwisho wake (vinywaji hiyo vinaleta harufu ya) miski. Na katika (kupata) haya washindane wenye kushindana

خِتَٰمُهُۥ مِسْكٌ ۚ وَفِى ذَٰلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ
ٱلْمُتَنَٰفِسُونَ ﴿٢٦﴾

27.Na mchanganyo wake ni (maji ya) Tasnymu.

وَمِزَاجُهُۥ مِن تَسْنِيمٍ ﴿٢٧﴾

28.(Hiyo tasnimu ni) chemchem watakayoinywa (watu) waliokurubishwa (na Mwenyezi Mungu).

عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا ٱلْمُقَرَّبُونَ ﴿٢٨﴾



Book3.indb 16 4/19/05 6:57:44 AM

| | |
|---|---|
| 29. Kwa hakika wote waliokuwa wanafanya madhambi walikuwa wakiwacheka walioamini. | إِنَّ الَّذِينَ أَجْرَمُوا كَانُوا مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا يَضْحَكُونَ ﴿٢٩﴾ |
| 30. Na wanapopita karibu yao wakikonyezana (kwa kuwachokoza). | وَإِذَا مَرُّوا بِهِمْ يَتَغَامَزُونَ ﴿٣٠﴾ |
| 31. Na wanaporudi kwa watu wao hurudi na hali ya kuwa wamefurahi (kwa kuwaudhi). | وَإِذَا انْقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمُ انْقَلَبُوا فَكِهِينَ ﴿٣١﴾ |
| 32. Na wanapowaona husema: "Hakika hawa ndio (khasa) waliopotea." | وَإِذَا رَأَوْهُمْ قَالُوا إِنَّ هَٰؤُلَاءِ لَضَالُّونَ ﴿٣٢﴾ |
| 33. Na wao makafiri hawakupelekwa kuwa walinzi juu yao (Waislamu). | وَمَا أُرْسِلُوا عَلَيْهِمْ حَافِظِينَ ﴿٣٣﴾ |
| 34. Basi leo walioamini watawacheka waliokufuru. | فَالْيَوْمَ الَّذِينَ آمَنُوا مِنَ الْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ ﴿٣٤﴾ |
| 35. Juu ya viti vya fakhari wakitazama (neema zao). | عَلَى الْأَرَائِكِ يَنْظُرُونَ ﴿٣٥﴾ |
| 36. Je, makafiri wamepewa malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda? | هَلْ ثُوِّبَ الْكُفَّارُ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾ |

ina aya 19 — **Suuratul Infitaar** — Makka

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

@

| | |
|---|---|
| 1. Mbingu zitakapo pasuka | إِذَا السَّمَاءُ انْفَطَرَتْ ﴿١﴾ |
| 2. Na nyota zitakapopukutika | وَإِذَا الْكَوَاكِبُ انْتَثَرَتْ ﴿٢﴾ |



Book3.indb 17 4/19/05 6:58:03 AM

| | |
|---|---|
| 3. Na bahari zitakapopasuliwa | وَإِذَا الْبِحَارُ فُجِّرَتْ ﴿٣﴾ |
| 4. Na makaburi yatakapofukuliwa | وَإِذَا الْقُبُورُ بُعْثِرَتْ ﴿٤﴾ |
| 5. (Kila) nafsi wakati (huo itajua) iliyoyatanguliza na iliyobakisha nyuma | عَلِمَتْ نَفْسٌ مَا قَدَّمَتْ وَأَخَّرَتْ ﴿٥﴾ |
| 6. Ee mwanaadamu! Ni nini kikudanganyacho na Mola wako mtukufu (hata ukamuasi)? | يَا أَيُّهَا الْإِنْسَانُ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ ﴿٦﴾ |
| 7. Aliyekuumba na kukutengeneza, kisha akakulinganisha sawa? | الَّذِي خَلَقَكَ فَسَوَّاكَ فَعَدَلَكَ ﴿٧﴾ |
| 8. Katika sura yoyote Aliyoipenda amekutengeneza. | فِي أَيِّ صُورَةٍ مَا شَاءَ رَكَّبَكَ ﴿٨﴾ |
| 9. Sivyo hivyo! Bali nyinyi mnakadhibisha Malipo. | كَلَّا بَلْ تُكَذِّبُونَ بِالدِّينِ ﴿٩﴾ |
| 10. Na hakika juu yenu kuna wenye kuwatunza | وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لَحَافِظِينَ ﴿١٠﴾ |
| 11. Watukufu wenye kuandika | كِرَامًا كَاتِبِينَ ﴿١١﴾ |
| 12. Wanayajua yote mnayoyatenda (na wanadhibiti) | يَعْلَمُونَ مَا تَفْعَلُونَ ﴿١٢﴾ |
| 13. Kwa hakika wafanyao wema watakuwa neemani. | إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿١٣﴾ |
| 14. Na waovu watakuwa Motoni. | وَإِنَّ الْفُجَّارَ لَفِي جَحِيمٍ ﴿١٤﴾ |
| 15. Wataingia humo siku ya malipo. | يَصْلَوْنَهَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٥﴾ |
| 16. Wala hawatatoka humo. | وَمَا هُمْ عَنْهَا بِغَائِبِينَ ﴿١٦﴾ |



Book3.indb 18 4/19/05 6:58:21 AM

17. Na nini kitakachojulisha siku ya malipo ni siku gani hiyo!

وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا يَوۡمُ ٱلدِّينِ ١٧

18. Tena nini kitakachojulisha siku ya malipo ni siku gani hiyo!

ثُمَّ مَآ أَدۡرَىٰكَ مَا يَوۡمُ ٱلدِّينِ ١٨

19. Ni siku ambayo nafsi haitaimiliki nafsi (nyingine) chochote; na amri siku hiyo itakuwa ya Mwenyezi Mungu (tu).

يَوۡمَ لَا تَمۡلِكُ نَفۡسٞ لِّنَفۡسٖ شَيۡـٔٗاۖ وَٱلۡأَمۡرُ يَوۡمَئِذٖ لِّلَّهِ ١٩

## aya 29 — Suuratu ttakwiir — Makka

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

1. Jua litakapokunjwa kunjwa

إِذَا ٱلشَّمۡسُ كُوِّرَتۡ ١

2. Na nyota zitakapopukutika

وَإِذَا ٱلنُّجُومُ ٱنكَدَرَتۡ ٢

3. Na milima itakapoendeshwa (angani kama vumbi).

وَإِذَا ٱلۡجِبَالُ سُيِّرَتۡ ٣

4. Na ngamia wenye mimba pevu watakapoachwa, (wasishughulikiwe).

وَإِذَا ٱلۡعِشَارُ عُطِّلَتۡ ٤

5. Na wanyama wa mwitu watakapokusanywa.

وَإِذَا ٱلۡوُحُوشُ حُشِرَتۡ ٥

6. Na bahari zitakapowashwa Moto.

وَإِذَا ٱلۡبِحَارُ سُجِّرَتۡ ٦

7. Na roho zitakapounganishwa (na viwiliwili vyake).

وَإِذَا ٱلنُّفُوسُ زُوِّجَتۡ ٧



Book3.indb 19 4/19/05 6:58:36 AM

| | |
|---|---|
| 8. Na mtoto mwanamke aliyezikwa hali ya kuwa yuhai atakapoulizwa. | وَإِذَا الْمَوْءُودَةُ سُئِلَتْ ﴿٨﴾ |
| 9. Kwa makosa gani aliuawa. | بِأَيِّ ذَنبٍ قُتِلَتْ ﴿٩﴾ |
| 10.Na madaftari (ya amali) yatakapoenezwa (kila mtu akapewa lake). | وَإِذَا الصُّحُفُ نُشِرَتْ ﴿١٠﴾ |
| 11.Na utando wa mbingu utakapotanduliwa. | وَإِذَا السَّمَاءُ كُشِطَتْ ﴿١١﴾ |
| 12.Na Jahannamu itakapochochewa. | وَإِذَا الْجَحِيمُ سُعِّرَتْ ﴿١٢﴾ |
| 13.Na Pepo itakaposogezwa. | وَإِذَا الْجَنَّةُ أُزْلِفَتْ ﴿١٣﴾ |
| 14.(Wakati huo) kila nafsi itajua ilichokihudhurisha, (amali ilizofanya). | عَلِمَتْ نَفْسٌ مَّا أَحْضَرَتْ ﴿١٤﴾ |
| 15.Basi naapa kwa nyota zinazorejea nyuma. | فَلَا أُقْسِمُ بِالْخُنَّسِ ﴿١٥﴾ |
| 16.Zinazokwenda, kisha zikajificha | الْجَوَارِ الْكُنَّسِ ﴿١٦﴾ |
| 17.Na kwa usiku uingiapo | وَاللَّيْلِ إِذَا عَسْعَسَ ﴿١٧﴾ |
| 18.Na kwa asubuhi inapopambazuka | وَالصُّبْحِ إِذَا تَنَفَّسَ ﴿١٨﴾ |
| 19.Na hakika hii (Qur-an) ni kauli (aliyokuja nayo) Mjumbe mtukufu (Jibril). | إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿١٩﴾ |
| 20.Mwenye nguvu, mwenye cheo cha hishima kwa Mwenyezi Mungu. | ذِي قُوَّةٍ عِندَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ﴿٢٠﴾ |

21.Anayetiiwa huko, kisha muaminifu.

مُّطَاعٍ ثَمَّ أَمِينٍ ﴿٢١﴾

22.Na kuwa mwenzenu (Muhammad) si mwendawazimu (kama mnavyomsingizia).

وَمَا صَاحِبُكُم بِمَجْنُونٍ ﴿٢٢﴾

23.Na hakika yeye alimuona (Jibril) katika upeo wa macho (mbinguni) ulio safi.

وَلَقَدْ رَآهُ بِالْأُفُقِ الْمُبِينِ ﴿٢٣﴾

24.Wala yeye si bakhili wa (kukuelezeni) mambo ya ghaibu.

وَمَا هُوَ عَلَى الْغَيْبِ بِضَنِينٍ ﴿٢٤﴾

25.Wala hii si kauli ya Shetani aliyefukuzwa katika rehma.

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ﴿٢٥﴾

26.Basi mnakwenda wapi?

فَأَيْنَ تَذْهَبُونَ ﴿٢٦﴾

27.Haikuwa hii Qur-an ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote.

إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعَالَمِينَ ﴿٢٧﴾

28.Kwa yule miongoni mwenu anayetaka kushika njia.

لِمَن شَاءَ مِنكُمْ أَن يَسْتَقِيمَ ﴿٢٨﴾

29.Wala nyinyi hamtataka isipokuwa atake Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote.

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٩﴾



Book3.indb 21 4/19/05 6:59:05 AM

# Suuratu Abasa

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

1. Alikunja (Mtume) uso na akapa nyongo.
   عَبَسَ وَتَوَلّٰىٓ ۝١
2. Kwa sababu alimjia kipofu.
   اَنْ جَآءَهُ الْاَعْمٰى ۝٢
3. Na nini kilichokujulisha (kuwa hahitaji mawaidha mapya)? Labda yeye atatakasika.
   وَمَا يُدْرِيْكَ لَعَلَّهٗ يَزَّكّٰىٓ ۝٣
4. Au atakumbuka (aliyoyasahau); ukumbusho huo upate kumfaa.
   اَوْ يَذَّكَّرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرٰى ۝٤
5. Ama ajionaye hana haja (ya dini).
   اَمَّا مَنِ اسْتَغْنٰى ۝٥
6. Wewe ndiye unayemshughulikia?
   فَاَنْتَ لَهٗ تَصَدّٰى ۝٦
7. Na si juu yako kama hakutakasika.
   وَمَا عَلَيْكَ اَلَّا يَزَّكّٰى ۝٧
8. Lakini anayekukimbilia.
   وَاَمَّا مَنْ جَآءَكَ يَسْعٰى ۝٨
9. Naye anaogopa.
   وَهُوَ يَخْشٰى ۝٩
10. Wewe unampuuza (Usifanye hivyo).
    فَاَنْتَ عَنْهُ تَلَهّٰى ۝١٠
11. Sivyo! Hakika (Qur-an) hii ni nasaha (mawaidha).
    كَلَّآ اِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ۝١١
12. Basi kila apendaye atawaidhika.
    فَمَنْ شَآءَ ذَكَرَهٗ ۝١٢
13. (Mawaidha haya yanatoka) katika kurasa zilizohishimiwa.
    فِيْ صُحُفٍ مُّكَرَّمَةٍ ۝١٣



Book3.indb 22 4/19/05 6:59:20 AM

| | |
|---|---|
| 14.Zilizotukuzwa, zilizotakaswa. | مَّرْفُوعَةٍ مُّطَهَّرَةٍ ﴿١٤﴾ |
| 15.Zilizomo mikononi mwa (Malaika) waandishi (wa Mwenyezi Mungu). | بِأَيْدِي سَفَرَةٍ ﴿١٥﴾ |
| 16.Watukufu, Waoha Mungu. | كِرَامٍ بَرَرَةٍ ﴿١٦﴾ |
| 17.Ameangamia Binaadamu namna gani ulivyo endelea mno ukafiri wake! | قُتِلَ الْإِنسَانُ مَا أَكْفَرَهُ ﴿١٧﴾ |
| 18.Kwa kitu gani Amemuumba? | مِنْ أَيِّ شَيْءٍ خَلَقَهُ ﴿١٨﴾ |
| 19.Kwa tone la manii; amemuumba akamuwezesha (akampa uweza) | مِن نُّطْفَةٍ خَلَقَهُ فَقَدَّرَهُ ﴿١٩﴾ |
| 20.Kisha akamfanyia njia nyepesi (ya kufanya mambo yake). | ثُمَّ السَّبِيلَ يَسَّرَهُ ﴿٢٠﴾ |
| 21.Kisha akamfisha na akamuweka kaburini | ثُمَّ أَمَاتَهُ فَأَقْبَرَهُ ﴿٢١﴾ |
| 22.Kisha Apendapo atamfufua. | ثُمَّ إِذَا شَاءَ أَنشَرَهُ ﴿٢٢﴾ |
| 23.La! Hajamaliza Aliyomuamuru (Mola wake). | كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَا أَمَرَهُ ﴿٢٣﴾ |
| 24.Hebu mwanaadamu na atazame chakula chake. | فَلْيَنظُرِ الْإِنسَانُ إِلَىٰ طَعَامِهِ ﴿٢٤﴾ |
| 25.Hakika Sisi tumemimina maji kwa nguvu (kutoka mawinguni): | أَنَّا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبًّا ﴿٢٥﴾ |
| 26.Tena tukaipasuapasua ardhi. | ثُمَّ شَقَقْنَا الْأَرْضَ شَقًّا ﴿٢٦﴾ |
| 27.Kisha Tukaotesha humo (vyakula vilivyo) chembe. | فَأَنبَتْنَا فِيهَا حَبًّا ﴿٢٧﴾ |
| 28. Na mizabibu na mboga | وَعِنَبًا وَقَضْبًا ﴿٢٨﴾ |

| | |
|---|---|
| 29.Na mizeituni na mitende. | وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا ﴿٢٩﴾ |
| 30.Na mabustani yenye miti iliyosongana barabara. | وَحَدَائِقَ غُلْبًا ﴿٣٠﴾ |
| 31.Na matunda na malisho. | وَفَاكِهَةً وَأَبًّا ﴿٣١﴾ |
| 32.Kwa ajili ya kukustarehesheni nyinyi na wanyama wenu. | مَتَاعًا لَكُمْ وَلِأَنْعَامِكُمْ ﴿٣٢﴾ |
| 33.Basi itakapokuja sauti kali iumizayo masikio, (sauti ya baragumu la Kiama) | فَإِذَا جَاءَتِ الصَّاخَّةُ ﴿٣٣﴾ |
| 34.Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye. | يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ﴿٣٤﴾ |
| 35.Na mamaye na babaye. | وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ ﴿٣٥﴾ |
| 36.Na mkewe na wanawe. | وَصَاحِبَتِهِ وَبَنِيهِ ﴿٣٦﴾ |
| 37.Kila mtu miongoni mwao Siku hiyo atakuwa na hali itakayomtosha mwenyewe, (hana haja ya mwenziwe). | لِكُلِّ امْرِئٍ مِنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ ﴿٣٧﴾ |
| 38.Siku hiyo nyuso nyingine zitanawiri. | وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ مُسْفِرَةٌ ﴿٣٨﴾ |
| 39.Zitacheka, zitachangamka. | ضَاحِكَةٌ مُسْتَبْشِرَةٌ ﴿٣٩﴾ |
| 40.Na nyuso nyingine Siku hiyo zitakuwa na mavumbi juu yake. | وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ عَلَيْهَا غَبَرَةٌ ﴿٤٠﴾ |
| 41.Giza totoro (kubwa) litazifunika. | تَرْهَقُهَا قَتَرَةٌ ﴿٤١﴾ |
| 42.Hao ndio makafiri watenda mabaya. | أُولَٰئِكَ هُمُ الْكَفَرَةُ الْفَجَرَةُ ﴿٤٢﴾ |



Book3.indb 24 4/19/05 6:59:56 AM

ina aya 46 **Suuratun Naaziaat** Makka

@

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

1. Naapa Kwa wote (Malaika) wavutao kwa nguvu (roho za watu wabaya).

وَالنّٰزِعٰتِ غَرْقًا ۙ ﴿١﴾

2. Na kwa wote wanaotoa (roho za watu wema) kwa ulatifu (taratibu).

وَّالنّٰشِطٰتِ نَشْطًا ۙ ﴿٢﴾

3. Wanaoogolea nazo (Wanaokwenda nazo mbio hizo roho).

وَّالسّٰبِحٰتِ سَبْحًا ۙ ﴿٣﴾

4. Wakazifikisha huko wanakozifikisha.

فَالسّٰبِقٰتِ سَبْقًا ۙ ﴿٤﴾

5. Wakazitengenezea mambo yake. (Mbaya zikaadhibiwa, na nzuri zikastareheshwa)

فَالْمُدَبِّرٰتِ اَمْرًا ۘ ﴿٥﴾

6. Siku litakapolia baragumu la mwanzo.

يَوْمَ تَرْجُفُ الرَّاجِفَةُ ۙ ﴿٦﴾

7. (Na) Lifuatiwe na baragumu la pili.

تَتْبَعُهَا الرَّادِفَةُ ۗ ﴿٧﴾

8. Siku hiyo nyoyo zitapigapiga (kwa khofu).

قُلُوْبٌ يَّوْمَئِذٍ وَّاجِفَةٌ ۙ ﴿٨﴾

9. Macho yake yatainamia chini.

اَبْصَارُهَا خَاشِعَةٌ ۘ ﴿٩﴾

10. (Makafiri) wanasema Je! Kweli tutarudishwa katika hali (yetu) ya kwanza? (Tutafufuliwa?).

يَقُوْلُوْنَ ءَاِنَّا لَمَرْدُوْدُوْنَ فِي الْحَافِرَةِ ۗ ﴿١٠﴾



Book3.indb 25 4/19/05 7:00:08 AM

| | |
|---|---|
| 11.Hata tukiwa mifupa mibovu. | ءَاِذَا كُنَّا عِظَامًا نَّخِرَةً ﴿١١﴾ |
| 12.Wanasema (kwa stihizai): "Basi marejeo haya ni yenye hasara (kwetu)." | قَالُوْا تِلْكَ اِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ﴿١٢﴾ |
| 13.Kwa hakika hicho (Kiama) kitakuwa (kwa kupigwa) ukelele mmoja tu. | فَاِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَّاحِدَةٌ ﴿١٣﴾ |
| 14.Mara wao (viumbe wote) watakuwa katika ardhi mpya. | فَاِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿١٤﴾ |
| 15.Je! Imekufikia hadithi ya Musa? | هَلْ اَتٰىكَ حَدِيْثُ مُوْسٰى ﴿١٥﴾ |
| 16.Mola wake alipomwita katika bonde takatifu (liitwalo) Tuwaa. | اِذْ نَادٰىهُ رَبُّهٗ بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٦﴾ |
| 17. Nenda kwa firauni; hakika yeye amezidi (jeuri). | اِذْهَبْ اِلٰى فِرْعَوْنَ اِنَّهٗ طَغٰى ﴿١٧﴾ |
| 18.Umwambie: Je, unapenda kujitakasa? | فَقُلْ هَلْ لَّكَ اِلٰٓى اَنْ تَزَكّٰى ﴿١٨﴾ |
| 19.Nami nitakuongoza kwa Mol wako ili umche. | وَاَهْدِيَكَ اِلٰى رَبِّكَ فَتَخْشٰى ﴿١٩﴾ |
| 20.Basi alimuonesha ishara kubwa-kubwa, (miujiza mikubwa mikubwa). | فَاَرٰىهُ الْاٰيَةَ الْكُبْرٰى ﴿٢٠﴾ |
| 21.Lakini alikadhibisha na akaasi. | فَكَذَّبَ وَعَصٰى ﴿٢١﴾ |
| 22.Kisha alirudi nyuma akaanza kufanya jitihadi (ya kuwazuilia watu wasimfuate Musa). | ثُمَّ اَدْبَرَ يَسْعٰى ﴿٢٢﴾ |
| 23.Basi aliwakusanya (watu) akanadi. | فَحَشَرَ فَنَادٰى ﴿٢٣﴾ |

| | |
|---|---|
| 24.Akasema: Mimi ndiye Mola wenu mkuu. | فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَىٰ ﴿٢٤﴾ |
| 25.Hapo Mwenyezi Mungu akamtia mkononi kwa kulipa tamko lake hili la mwisho na kwa lile tamko lake la mwanzo. | فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْآخِرَةِ وَالْأُولَىٰ ﴿٢٥﴾ |
| 26.Kwa hakika katika haya limo onyo (kubwa) kwa wote wanaoogopa. | إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَعِبْرَةً لِّمَن يَخْشَىٰ ﴿٢٦﴾ |
| 27.Je, nyinyi ni wenye umbo la nguvu zaidi au mbingu? Yeye amezijenga. | ءَأَنتُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءُ بَنَاهَا ﴿٢٧﴾ |
| 28.Akainua kimo chake na akazitengeneza vizuri. | رَفَعَ سَمْكَهَا فَسَوَّاهَا ﴿٢٨﴾ |
| 29.Na akautia giza usiku wake na kautokezesha mchana wake. | وَأَغْطَشَ لَيْلَهَا وَأَخْرَجَ ضُحَاهَا ﴿٢٩﴾ |
| 30.Na ardhi baada ya hayo akaitandaza. | وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَٰلِكَ دَحَاهَا ﴿٣٠﴾ |
| 31.Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake. | أَخْرَجَ مِنْهَا مَاءَهَا وَمَرْعَاهَا ﴿٣١﴾ |
| 32.Na milima akaisimamisha. | وَالْجِبَالَ أَرْسَاهَا ﴿٣٢﴾ |
| 33.Kwa ajili ya kukustarehesheni nyinyi na wanyama wenu. | مَتَاعًا لَّكُمْ وَلِأَنْعَامِكُمْ ﴿٣٣﴾ |
| 34.Basi itakapofika hiyo balaa kubwa (ya Kiama). | فَإِذَا جَاءَتِ الطَّامَّةُ الْكُبْرَىٰ ﴿٣٤﴾ |
| 35.Siku ambayo mtu atakumbuka kila alililofanya. | يَوْمَ يَتَذَكَّرُ الْإِنسَانُ مَا سَعَىٰ ﴿٣٥﴾ |
| 36.Na Moto mkali utaoneshwa kwa kila aonaye. | وَبُرِّزَتِ الْجَحِيمُ لِمَن يَرَىٰ ﴿٣٦﴾ |



Book3.indb 27 4/19/05 7:00:47 AM

| | |
|---|---|
| 37.Ama yule aliyeasi. | فَاَمَّا مَنْ طَغٰى ﴿۳۷﴾ |
| 38.Na akapenda zaidi, (maisha ya dunia). | وَاٰثَرَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا ﴿۳۸﴾ |
| 39.Basi kwa hakika Jahannamu ndiyo itakayokuwa makazi yake. | فَاِنَّ الْجَحِيْمَ هِيَ الْمَاْوٰى ﴿۳۹﴾ |
| 40.Na ama yule aliyeogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake, akaikataza nafsi yake na matamanio (maovu). | وَاَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهٖ وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوٰى ﴿۴۰﴾ |
| 41.Basi (huyo) Pepo ndiyo itakayokuwa makazi yake. | فَاِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ الْمَاْوٰى ﴿۴۱﴾ |
| 42.Wanakuuliza Kiama kutokea kwake kutakuwa lini? | يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ السَّاعَةِ اَيَّانَ مُرْسٰىهَا ﴿۴۲﴾ |
| 43.Uko wapi na kuweza kutaja (wakati wa kuja Kiama)? | فِيْمَ اَنْتَ مِنْ ذِكْرٰىهَا ﴿۴۳﴾ |
| 44.Mwisho (wa ujuzi) wake uko kwa Mola wako. | اِلٰى رَبِّكَ مُنْتَهٰىهَا ﴿۴۴﴾ |
| 45.Wewe ni Muonyaji (tu) kwa yule anayekiogopa. | اِنَّمَآ اَنْتَ مُنْذِرُ مَنْ يَّخْشٰىهَا ﴿۴۵﴾ |
| 46.Siku watakapokiona watakuwa kana kwamba hawakukaa (ulimwenguni) ila jioni moja au mchana wake | كَاَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوْٓا اِلَّا عَشِيَّةً اَوْ ضُحٰىهَا ﴿۴۶﴾ |



Book3.indb 28 4/19/05 7:01:03 AM

aya 40

## Suuratun Nabai

Makka

*Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu*

| | |
|---|---|
| 1. Wanaulizana habari gani? | عَمَّ يَتَسَآءَلُونَ ﴿١﴾ |
| 2. Ile habari iliyo kuu (ya kufufuliwa viumbe). | عَنِ النَّبَإِ الْعَظِيمِ ﴿٢﴾ |
| 3. Ambayo wanakhitalifiana. | الَّذِى هُمْ فِيهِ مُخْتَلِفُونَ ﴿٣﴾ |
| 4. Nawakome! (wasikhitalifiane). Hivi karibuni watajua (ukweli wake). | كَلَّا سَيَعْلَمُونَ ﴿٤﴾ |
| 5. Kisha nawakome! Hivi karibuni watajua (ukweli wake). | ثُمَّ كَلَّا سَيَعْلَمُونَ ﴿٥﴾ |
| 6. Je! Hatukuifanya ardhi kuwa tandiko. | أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ مِهٰدًا ﴿٦﴾ |
| 7. Na milima kuwa kama vigingi (vya ardhi)? | وَالْجِبَالَ أَوْتَادًا ﴿٧﴾ |
| 8. Na tukakuumbeni wanaume na wanawake. | وَخَلَقْنٰكُمْ أَزْوٰجًا ﴿٨﴾ |
| 9. Na tukaufanya usingizi wenu kama kufa. | وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا ﴿٩﴾ |
| 10. Na tukaufanya usiku kama nguo (mnalofunikwa). | وَجَعَلْنَا الَّيْلَ لِبَاسًا ﴿١٠﴾ |
| 11. Na tukaufanya mchana kama kufufuka. | وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ﴿١١﴾ |
| 12. Na tukajenga juu yenu (mbingu) saba madhubuti. | وَبَنَيْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعًا شِدَادًا ﴿١٢﴾ |



Book3.indb 29 4/19/05 7:01:17 AM

| | |
|---|---|
| 13. Na tukaifanya taa ing'arayo na yenye joto kubwa. | وَّجَعَلْنَا سِرَاجًا وَّهَّاجًا ۝١٣ |
| 14. Na tukateremsha maji yaangukayo kwa kasi kutoka mawinguni. | وَّاَنْزَلْنَا مِنَ الْمُعْصِرٰتِ مَآءً ثَجَّاجًا ۝١٤ |
| 15. Ili kwayo tuoteshe (vyakula vilivyo) chembe chembe na mimea (mengine). | لِّنُخْرِجَ بِهٖ حَبًّا وَّنَبَاتًا ۝١٥ |
| 16. Na mabustani yenye miti iliyosongana. | وَّجَنّٰتٍ اَلْفَافًا ۝١٦ |
| 17. Kwa hakika siku ya Hukumu imewekewa wakati maalumu. | اِنَّ يَوْمَ الْفَصْلِ كَانَ مِيْقَاتًا ۝١٧ |
| 18. Siku itakapopigwa parapanda (baragumu), nanyi mtafika makundi makundi. | يَّوْمَ يُنْفَخُ فِى الصُّوْرِ فَتَاْتُوْنَ اَفْوَاجًا ۝١٨ |
| 19. Na mbingu zitafunguliwa ziwe milango milango. | وَّفُتِحَتِ السَّمَآءُ فَكَانَتْ اَبْوَابًا ۝١٩ |
| 20. Na milima itaondolewa na itakuwa kama mangati (kama maji ukiyaangaalia kwa mbali). | وَّسُيِّرَتِ الْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا ۝٢٠ |
| 21. Kwa hakika Jahannamu inawangoja wabaya. | اِنَّ جَهَنَّمَ كَانَتْ مِرْصَادًا ۝٢١ |
| 22. Ni makazi ya maasi. | لِّلطّٰغِيْنَ مَاٰبًا ۝٢٢ |
| 23. Wakae humo dahari nyingi (karne baada ya karne). | لّٰبِثِيْنَ فِيْهَآ اَحْقَابًا ۝٢٣ |
| 24. Hawataonja humo baridi wala kinywaji. | لَا يَذُوْقُوْنَ فِيْهَا بَرْدًا وَّلَا شَرَابًا ۝٢٤ |
| 25. Ila maji yachemkayo sana na usaha. | اِلَّا حَمِيْمًا وَّغَسَّاقًا ۝٢٥ |



Book3.indb 30 4/19/05 7:01:36 AM

26.(Wanalipwa) Malipo yaliyo sawa (na amali zao).

جَزَآءً وِفَاقًا ﴿٢٦﴾

27.Hakika wao hawakuwa wakiogopa hisabu.

إِنَّهُمْ كَانُوا لَا يَرْجُونَ حِسَابًا ﴿٢٧﴾

28.Na walikuwa wakikadhibisha Aya zetu kukadhibisha.

وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كِذَّابًا ﴿٢٨﴾

29.Na (Hali ya kuwa) kila kitu tumekidhibiti kwa kukiandika.

وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ كِتَابًا ﴿٢٩﴾

30.Basi onjeni. Nasi Hatutakuzidishieni ila adhabu (juu ya adhabu).

فَذُوقُوا فَلَن نَّزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٣٠﴾

31.Hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu wamefuzu.

إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ مَفَازًا ﴿٣١﴾

32.Mabustani na mizabibu.

حَدَائِقَ وَأَعْنَابًا ﴿٣٢﴾

33.Na wanawake vijana walio hirimu (na waume zao).

وَكَوَاعِبَ أَتْرَابًا ﴿٣٣﴾

34.Na gilasi zilizojaa (vinywaji vizuri vizuri).

وَكَأْسًا دِهَاقًا ﴿٣٤﴾

35.Hawatasikia humo upuuzi wala ya kukadhibishana.

لَّا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا كِذَّابًا ﴿٣٥﴾

36.Watalipwa kutoka kwa Mola wako atia yenye kutosha.

جَزَاءً مِّن رَّبِّكَ عَطَاءً حِسَابًا ﴿٣٦﴾

37.Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake, Mwingi wa Rehema hutaweza kusema naye.

رَّبِّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا الرَّحْمَٰنِ لَا يَمْلِكُونَ مِنْهُ خِطَابًا ﴿٣٧﴾



Book3.indb 31 4/19/05 7:01:55 AM

**38.Siku ambayo zitasimama roho na Malaika safusafu, hatasema siku hiyo ila yule ambaye Mwingi wa Rehema amempa idhini na atasema yaliyo sawa.**

يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلَٰٓئِكَةُ صَفًّا ۖ
لَّا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أَذِنَ لَهُ الرَّحْمَٰنُ
وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾

**39.Hiyo ndiyo siku ya haki, basi anayetaka na ashike njia aende kwa Mola wake.**

ذَٰلِكَ الْيَوْمُ الْحَقُّ ۖ فَمَن شَآءَ
اتَّخَذَ إِلَىٰ رَبِّهِۦ مَـَٔابًا ﴿٣٩﴾

**40.Hakika tunakuhadharisheni adhabu iliyo karibu. Siku ambayo mtu atakapoona yaliyotangulizwa na mikono yake miwili, na kafiri atasema: Laiti ningalikuwa udongo.**

إِنَّآ أَنذَرْنَٰكُمْ عَذَابًا قَرِيبًا
يَوْمَ يَنظُرُ الْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ
وَيَقُولُ الْكَافِرُ يَٰلَيْتَنِى كُنتُ تُرَٰبًۢا ﴿٤٠﴾



Book3.indb 32 4/19/05 7:02:07 AM

# Somo la 2. Tawhid

## IMANI YA KIISLAMU

**NGUZO ZA IMANI**

Imani ya kiislamu imejengwa juu ya nguzo sita. Hawi muumini wa kweli muislamu asiyeamini nguzo hizi kwa pamoja au yule aaminiye baadhi ya nguzo hizi.Uislamu ni dini iliyojengwa juu ya nguzo sita za Imani kama zifuatazo:

1. Kumuamini Allah.
2. Kuwaamini Malaika wa Allah.
3. Kuamini vitabu vya Allah.
4. Kuamini Mitume wa Allah.
5. Kuamini siku ya mwisho
6. Kuamini Qadar ya Allah.

Tunazifahamu nguzo hizi kutokana na hadithi ya Mtume (s.a.w). Amesimulia Umar (r.a) kuwa Mtume (s.a.w) amesema:

> *"Imani ni kumuamini Allah na Malaika wake na vitabu vyake na Mitume wake na siku ya mwisho na Qadar yake". (Muslim).*

Katika aya ifuatayo zinatajwa kwa mfululizo nguzo nne za kwanza:

ءَامَنَ ٱلرَّسُولُ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيۡهِ مِن رَّبِّهِۦ وَٱلۡمُؤۡمِنُونَۚ
كُلٌّ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَكُتُبِهِۦ وَرُسُلِهِۦ لَا نُفَرِّقُ
بَيۡنَ أَحَدٖ مِّن رُّسُلِهِۦۚ ﴿٢٨٥﴾

> *"Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake na Waislamu, (Pia wameamini hayo): wote wamemwamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume yake; (nao hao Waislamu na Mtume wao husema), "Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume yake (wote tunawaamni)"... (2:285).*


Book3.indb 33 4/19/05 7:02:42 AM

Pia katika aya ifuatayo zimetajwa nguzo tano za kwanza kwa mfululizo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ ءَامِنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَٱلْكِتَٰبِ
ٱلَّذِى نَزَّلَ عَلَىٰ رَسُولِهِۦ وَٱلْكِتَٰبِ ٱلَّذِىٓ أَنزَلَ مِن
قَبْلُ ۚ وَمَن يَكْفُرْ بِٱللَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَكُتُبِهِۦ وَرُسُلِهِۦ وَٱلْيَوْمِ
ٱلْءَاخِرِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًۢا بَعِيدًا ﴿١٣٦﴾

*Enyi mlioamini! Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Kitabu alichokiteremsha juu ya Mtume wake, na Vitabu alivyoviteremsha zamani. Na Mwenye kumkanusha Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na siku ya mwisho, basi bila shaka amepotea upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki). (4:136).*

Nguzo ya sita ya kuamini Qadar imebainishwa katika aya mbali mbali za Qur-an kama vile:

مَآ أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِى ٱلْأَرْضِ وَلَا فِىٓ أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِى
كِتَٰبٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَآ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ
يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾

*Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwishaandikwa katika* Kitabu *(cha Mwenyezi Mungu) kabla hatujauumba. Kwa yakini hilo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu (57:2).*

**KUMUAMINI ALLAH (S.W)**

Baada ya kujiuliza maswali mengi katika kitabu cha kwanza na cha pili tulihitimisha kuwa:

Allah ndiye Muumba wa mbingu na vyote vilivyomo katika anga, ndiye aliyeumba jua, mwezi, nyota na sayari mbali mbali katika anga.

Allah ndiye Muumba wa ardhi na vilivyomo ndani yake. Ndiye aliyeumba mito, bahari maziwa, milima na mabonde.



Book3.indb 34 4/19/05 7:03:01 AM

Allah ndiye aliye waumba watu, wanyama na viumbe vyote vilivyo hai vya barani na baharini.

Allah ndiye chanzo cha uhai wa watu, wanyama, mimea na wa kila kilicho hai.

Allah pekee ndiye anayestahiki kusifiwa kwa sifa zote tukufu. Yeye pekee ndiye anayestahiki kushukuriwa na kutiiwa kwa unyenyekevu na wote wenye kutumia akili zao vizuri.

**Dalili za kuwepo Allah (s.w) kutokana na Mwanaadamu**

Katika kitabu cha kwanza na cha pili tulizingatia umbile la mbingu na ardhi na vilivyomo kama vile jua, mwezi, nyota, watu, wanyama, mimea, milima, mito, bahari na kadhalika katika kuthibitisha kuwepo kwa Allah (s.w).

Kwa kuzingatia dalili hizo tuliona kuwa ni lazima pawe na Muumbaji aliyemuweza na mjuzi kweli kweli. Tukathibitisha kuwa muumbaji huyu ni Allah (s.w). Naye ndiye aliyekipa uhai kila chenye uhai.

Hebu katika kitabu hiki tumtafakari mwanaadamu kama dalili nyingine ya kuwepo Allah (s.w).

**Chanzo cha watu**

Tunajifunza katika Qur-an kuwa mtu wa kwanza ni Adam (a.s). Ni nani aliyemuumba Adam? Tena tunafahamishwa katika Qur-an kuwa Adam ametengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi. Je, pamoja na ujanja wetu wote, tunaweza kumtengeneza mtu kwa udongo wa mfinyazi? Tunachoweza ni kutengeneza sanamu la mtu kwa udongo au shaba.



Kuna masanamu mengi ya Askari katika miji mbali mbali ya Tanzania. Zanzibar kuna sanamu la Abeid Karume na kule Tabora kuna sanamu la Mwalimu Nyerere.

Lakini je, kuna anayeweza kuyapa uhai?



Book3.indb 35 4/19/05 7:03:02 AM

Nani aliyelipa sanamu la Adam uhai? Bila shaka aliyemuumba Adam kutokana na udongo na kumpulizia roho ni Allah (s.w) kama anavyotufahamisha katika Qur-an:

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِندَ ٱللَّهِ كَمَثَلِ ءَادَمَ ۖ خَلَقَهُۥ مِن تُرَابٍ
ثُمَّ قَالَ لَهُۥ كُن فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾

*Bila shaka hali ya Issa kwa Allah ni kama hali ya Adam. Alimuumba kwa udongo kisha akamwambia, "Kuwa" basi akawa". (3:59).*

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَٰٓئِكَةِ إِنِّى خَٰلِقٌۢ بَشَرًا مِّن صَلْصَٰلٍ مِّنْ
حَمَإٍ مَّسْنُونٍ ﴿٢٨﴾ فَإِذَا سَوَّيْتُهُۥ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِى
فَقَعُوا۟ لَهُۥ سَٰجِدِينَ ﴿٢٩﴾

*"Na kumbukeni Mola wako alipowaambia Malaika, Hakika mimi nitamuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti, wenye kutokana na matope meusi, yaliyovunda. Basi nitakapomkamilisha na kumpulizia roho itokanayo na Mimi, bai msujudieni" (15:28-29).*

Baada ya kuumbwa Adam (a.s), mwanaume wa kwanza, alifuatia kuumbwa Hawwa, mwanamke wa kwanza. Hawa wawili waliozeshwa na Mola wao na kuwa baba na mama wa mwanzo. Walizaa watoto na vizazi vyao vinaendelea mpaka leo. Leo hii watu wanajulikana kwa jina la wanaadamu yaani Wana wa Adam. Allah (s.w) anatukumbusha katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَٰكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ

*Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni nyote kwa yule mwanamume wa kwanza (Adamu) na yule mwanamke (wa kwanza Hawwa).... (49:13)*

Ni nani anayemtengeneza mtoto tumboni mwa mama na kumpa uhai. Je, ni baba au mama anayefanya kazi hii?



Book3.indb 36 4/19/05 7:03:24 AM



Baba na mama hawana uwezo. Nani basi anayeifanya kazi hiyo? Bila shaka si mwingine bali ni Allah (s.w).

**Lishe ya mtoto mchanga**

Mtoto mchanga hawezi kula chakula. Hunyonya maziwa ya mama yake tu. Nani aliyetengeneza maziwa hayo? Nani aliyemfundisha mtoto kunyonya? Baada ya mtoto kutoa meno huanza kula vyakula vigumu. Nani aliyempa mtoto meno? Bila shaka aliyeweka taratibu za lishe ya mtoto mchanga ni Muumba wake – Allah (s.w).






Book3.indb 37 4/19/05 7:03:26 AM

**Kukua kwa mtoto**

Kukua kwa mtoto hadi kufikia ujana na hatimaye kuwa mtu mzee kikongwe ni dalili nyingine ya kuwepo Allah (s.w).




Picha ya (1) hadi ya (8) zinatuonyesha hatua anazopita mwanaadamu katika kukua kwake.

Nani anayeongoza makuzi ya mtoto? Si baba wala mama anayemkuza mtoto? Mtoto mwenyewe hana uwezo wa kujikuza. Nani basi anayemkuza mtoto mpaka kufikia hatua ya uzeeni? Bila shaka anayemkuza mtoto ni Allah (s.w) kama anavyotufahamisha katika Qur-an:

وَنُقِرُّ فِي ٱلۡأَرۡحَامِ مَا نَشَآءُ إِلَىٰٓ أَجَلٖ مُّسَمّٗى ثُمَّ نُخۡرِجُكُمۡ
طِفۡلٗا ثُمَّ لِتَبۡلُغُوٓاْ أَشُدَّكُمۡۖ وَمِنكُم مَّن يُتَوَفَّىٰ
وَمِنكُم مَّن يُرَدُّ إِلَىٰٓ أَرۡذَلِ ٱلۡعُمُرِ لِكَيۡلَا يَعۡلَمَ مِنۢ
بَعۡدِ عِلۡمٖ شَيۡـٔٗاۚ


*"… Nasi tunakikalisha matumboni tunachokitaka mpaka muda uliowekwa, kisha tunakutoeni kwa hali ya utoto; kisha tunakuleeni ili mfikie baleghe yenu. Na kuna wanaokufa kabla ya kufikia hali hii. Na katika nyinyi wako wanaorudishwa katika umri dhalili asijue chochote baada ya kule kujua kwake… (22:5).*

**Umbile la mwanaadamu na sura yake**

Nani aliyemfinyanga mtu na kumremba kama alivyo? Hebu jiangalie katika kioo. Hebu angalia vidole vyako na mwili wako kwa ujumla ulivyosawazishwa. Bila shaka mwanaadamu ameumbwa na Mola wake katika umbo lililo bora kabisa.

لَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ فِيٓ أَحۡسَنِ تَقۡوِيمٖ ٤

*"Bila shaka tumemuumba mwanaadamu kwa umbo lililo bora kabisa" (95:4).*





Book3.indb 39 4/19/05 7:03:40 AM

Pia Allah (s.w) anatutanabahisha katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡإِنسَٰنُ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ ٱلۡكَرِيمِ ٦ ٱلَّذِي خَلَقَكَ
فَسَوَّىٰكَ فَعَدَلَكَ ٧ فِيٓ أَيِّ صُورَةٖ مَّا شَآءَ رَكَّبَكَ ٨

*"Ee Mwanaadamu! Ni nini kikudanganyacho (hata ukamuasi) Mola wako Mtukufu? Aliyekuumba na kukutengeneza kisha akakulinganisha sawa sawa. Katika sura yoyote aliyoipenda amekutengeneza." (82:6-8).*

**Mgawanyiko wa watu katika rangi, makabila na Mataifa**

Taifa la Tanzania limegawanyika katika makabila mengi. Yako makabila zaidi ya 120 hapa Tanzania. Kila mmoja katika sisis anatokana na kabila moja au jingine. Ni nani aliyewagawanya watu kwenye makabila mbali mbali? Je, haya makabila watu wanayabuni wenyewe? Kila kabila lina zungumza lugha yake. Nani mtunzi wa lugha hizi? Je, kuna anayemfunza mtoto kuzungumza lugha ya mama yake?



Duniani kuna mataifa mengi na kuna watu wenye rangi mbali mbali na lugha mbali mbali.

Nani msanii wa makabila, mataifa, lugha na rangi za watu? Bila shaka msanii wa wa vyote hivi ni Allah (s.w) kama Qur-an inavyotuthibitishia:



Book3.indb 40 4/19/05 7:03:47 AM

وَجَعَلْنَٰكُمْ شُعُوبًا وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓا۟


*"… Na tumekufanyeni, mataifa na makabila mbali mbali ili mjuane (tu basi)… (49:13)*

وَمِنْ ءَايَٰتِهِۦ خَلْقُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَٱخْتِلَٰفُ أَلْسِنَتِكُمْ وَأَلْوَٰنِكُمْ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَءَايَٰتٍ لِّلْعَٰلِمِينَ ۝

*"Na katika ishara zake (za kuonyesha uwezo wake) ni kuumba mbingu na ardhi, na kutofautiana lugha zenu na rangi zenu. Kwa yakini katika haya zimo ishara kwa wenye ujuzi." (30:22).*

**Usingizi**

Tunalala kila siku. Nani anayeleta usingizi? Ni mtu mwenyewe anayetengeneza usingizi? Kweli ni kwamba hatuujui usingizi ulivyo wala hatuutengenezi sisi. Bali tunajikuta tu tumelala.



Bila shaka anayeleta usingizi ni Allah (s.w) kama anavyotufahamisha katika Qur-an:




Book3.indb 41 4/19/05 7:03:58 AM

وَمِنْ ءَايَـٰتِهِۦ مَنَامُكُم بِٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ وَٱبْتِغَآؤُكُم مِّن فَضْلِهِۦٓ ۚ
إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَءَايَـٰتٍ لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٢٣﴾

*"Na katika ishara zake ni kulala kwenu usiku na (kuamka) mchana, na kutafuta fadhila yake. Hakika katika hayo zimo ishara kwa watu wanaosikia."* (30:23).

**Kifo**

Sisi sote hatupendi kufa wala hatupendi jamaa zetu na rafiki zetu wafe. Lakini bado kifo kinaipitia kila nyumba. Sisi tutakufa lakini hatujui ni lini. Nani anayeleta kifo?



Anayefisha ni Allah (s.w) kama anavyotukumbusha katika Qur-an:



Book3.indb 42 4/19/05 7:04:05 AM

ثُمَّ إِنَّكُم بَعْدَ ذَٰلِكَ لَمَيِّتُونَ ﴿١٥﴾

*"Kisha hakika nyinyi baada ya hayo ni wenye kufa" (23:15).*

Katika aya nyingine anatufahamisha:

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ ۖ ثُمَّ إِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٥٧﴾

*"Kila nafsi itaonja mauti, kisha mtarudishwa kwetu" (29:57).*

Ni jambo la hakika kuwa mwanadamu hakujiumba mwenyewe na wala hakuna mtu aliyemumba mwenzake. Binadamu wote wameumbwa na Allah (s.w). Kutokana na haya machache tuliyojifunza tumefahamu kuwa mwanaadamu mwenyewe ni dalili tosha ya kuwepo Allah (s.w) na uweza wake.



Book3.indb 43 4/19/05 7:04:10 AM



## Zoezi la Pili

1.Imani ya kiislamu imejengwa juu ya nguzo..............

2. Hawi muumini wa kweli asiyeamini:

(a).............................................................................

(b).............................................................................

(c).............................................................................

(d).............................................................................

(e).............................................................................

(f).............................................................................

3. Taja dalili zinazoonesha kuwepo Allah(s.w) kutokana na maisha ya mw anadamu.

4. Toa sababu ni kwanini mambo hayo uliyoyataja hapo juu yanaonesha kuwa Allah(s.w) yupo?



Book3.indb 44 4/19/05 7:04:10 AM

# NGUZO ZA UISLAMU

**MISINGI YA NGUZO ZA UISLAMU**

Kama ilivyokuwa kwa nguzo za imani, nguzo za uislamu zimebainishwa katika Quran tukufu na Hadith za Mtume Muhammad (s.w). Abdillah ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa 'Allah (s.w) amesema: Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano:

1. Kushuhudia kuwa hapana Mola ila Allah, na kushuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah (s.w).
2. Kusimamisha swala tano.
3. Kutoa Zakati kwa Mwenye mali.
4. Kufunga mwezi wa Ramadhani.
5. Kuhiji Makka kwa kila mwenye uwezo wa kwenda huko.

Uislamu umefananishwa na jengo kubwa. Jengo hili limesimamishwa na nguzo tano. Nguzo moja tu ikiondolewa jengo linaporomoka. Hivyo Muislamu akivunja nguzo moja ya Uislamu. Uislamu wake huporomoka. Hii ina maana kuwa:

- Muislamu asiyesimamisha swala tano, ameuvunja Uislamu wake.
- Muislamu anayeacha kufunga ameuvunja Uislamu wake.
- Muislamu asiyetoa Zakat na huku ana mali amevunja Uislamu wake.
- Muislamu asiyekwenda kuhiji na huku ana uwezo wa mali na afya, amevunja Uislamu wake.

Hakuna Uislamu wa nguzo moja au mbili au tatu au nne. Uislamu husimama kwa kusimamisha nguzo zote tano kwa kadiri ya uwezo. Baba na Mama ni waislamu wa kweli. Wanatekeleza nguzo zote za Uislamu.

Mimi ni Muislamu. Nimeshahadia. Nina simamisha swala tano kila siku. Ninafunga mwezi wa Ramdhani kila mwaka. Insha-Allah nikipata mali na uwezo nitatoa Zakati na kwenda kuhiji Makka.



Book3.indb 45 4/19/05 7:04:11 AM

اَشْهَدُ اَنْ لآ اِلٰهَ إِلَّ اللّٰهُ وَاَشْهَدُ اَنَّ مُحَمَّدًا رَسُوْلُ اللّٰهُ

*Nashuhudia kuwa hapana Mola ila Allah. Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah.*

Asiyekuwa Muislamu huingia Uislamu kwa kutoa shahada mbili. Waislamu ulimwengu mzima hukumbushwa shahada katika adhana mara kumi kwa siku. Kila Muislamu wa kweli hushahadia mara tisa na zaidi kwa siku. Mtu anayekaribia kufa hutamkiwa shahada.

**Kushahadia kwa vitendo**

Shahada ndio roho ya Uislamu. Shahada huupa Uislamu uhai. Mtu aliyetoa shahada ya kweli muda wote humnyenyekea na kumtii Allah (s.w) na Mtume wake.

Kumnyenyekea na kumtii Allah (s.w) ni kufuata maamrisho yote ya Allah (s.w) na kuacha makatazo yake yote. Maamrisho ya Allah (s.w) ni mengi na yamebainishwa katika Quran tukufu. Miongoni mwa maamrisho ya Allah ni kusimamisha Swala, kutoa zakati, kufunga ?Ramadhani, Kuhiji Makka, kuwatii wazazi, kuwaheshimu watu, kusema ukweli, kuwasaidia wenye shida, kukaa na watu kwa wema na kadhalika.

Makatazo ya Allah (s.w) pia ni mengi na yamebainishwa katika Qur-an tukufu. Miongnani mwa makatazo ya Allah (s.w) ni kusema uwongo, kusengenya, kufitinisha watu, kutukana, kudharau wengine, majivuno, kuiba, kulewa, na kadhalika.

Kumnyenyekea na kumtii Mtume Muhammad (s.a.w) ni kufuata yale yote aliyotuamrisha na kuacha yale yote aliyotukutaza. Mtume (s.a.w) ametuamrisha yale yote aliyotuamrisha Allah na ametukataza yale yote aliyotukaza Allah. Juu ya kumtii Mtume, Allah (s.w) anatuamrisha:

وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمْ عَنْهُ فَٱنتَهُوا۟

*"... Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho..." (59:7)*



Book3.indb 46 4/19/05 7:04:20 AM

Mtume (s.a.w) mwenyewe alikuwa akimnyenyekea na kumtii Allah (s.w) kuliko mtu yoyote yule.

Pia Mtume (s.a.w) alikuwa na tabia njema kuliko mtu yoyote yule. Alikuwa mpole na mwenye huruma kwa watu wote na hata wanyama. Alikuwa mwenye upendo, mkarimu, msamehevu, mkweli, mwaminifu, mwadilifu, mwenye ahadi, shujaa, jasiri, mcheshi na mcha-Mungu kuliko mtu yoyote yule. Allah (s.w) ameisifu tabia ya Mtume (s.a.w) katika Qur-an:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

*"Na bila shaka unatabia njema kabisa" (68:4)*

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ

*"Bila shaka mnao mfano mwema kwa mtume wa Mwenyezi Mungu… (33:21).*

**Mnafiki**

Mnafiki ni yule anayetoa shahada ya uwongo. Anasema mdomoni,"Na shuhudia kuwa hapana Mola wa haki ila Allah, na nashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah" . Lakini katika utendaji hafuati maamrisho ya Allah na Mtume wake. Wala haachi yale aliyoyakataza Allah (s.w) na Mtume wake. Mnafiki hushirikiana na Kafiri katika kumuasi Allah na Mtume wake. Kafiri ni yule anayemkanusha Allah (s.w) na Mitume wake.

Mnafiki hutoa siri za waislamu kwa makafiri. Husaidiana na makafiri katika kuuhujumu Uislamu na waislamu. Wanafiki ni watu wabaya sana. Wameahidiwa adhabu kali na Allah (s.w) huko Akhera.

إِنَّ ٱلْمُنَٰفِقِينَ فِي ٱلدَّرْكِ ٱلْأَسْفَلِ مِنَ ٱلنَّارِ وَلَن تَجِدَ
لَهُمْ نَصِيرًا ﴿١٤٥﴾

*"Bila shaka wanafiki watakuwa katika tabaka la chini kabisa katika moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi (yoyote)". (4:145).*



Book3.indb 47 4/19/05 7:04:31 AM

**Twahara**

Twahara ni jambo muhimu sana katika Uislamu. Umuhimu wake unabainishwa na kauli ya Mtume (s.a.w): "Ufunguo wa Pepo ni swala na ufunguo wa swala ni Twahara". Muislamu aliyetwaharika kiasi cha kuweza kuswali ni yule aliyeepukana na najisi.

**Najisi**

Najisi ni uchafu. Kuna aina kubwa mbili za Najisi. Najisi ndogo na Najisi Kubwa.

**Najisi ndogo ni**

(1) Haja ndogo (mkojo)
(2) Haja kubwa (kinyesi).
(3) Damu.
(4) Matapishi.
(5) Usaha.
(6) Mzoga wowote ila samaki, nzige na maiti ya binaadamu.
(7) Kiungo cha mnyama kilichokatwa yungali hai.
(8) Maziwa ya mnyama asiyeliwa.
(9) Ulevi (pombe za aina zote).

**Najisi kubwa ni**

(1) Mbwa na mate yake, kinyesi chake, mkojo wake, manyoya yake, na kila chake (kila kinachotokana na mbwa).
(2) Nguruwe na kila chake (kila kinachotokana na nguruwe).

Huwezi kuswali mpaka uepukane na aina zote za najisi katika mwili, nguo na mahali pa kuswalia. Najisi huondoshwa kwa kutumia maji safi.

**Kuondosha Najisi Ndogo**

Ukisafisha nguo yako kutokana na najisi ndogo, zingatia utaratibu ufuatao:

(1) Mimina maji yapitie sehemu yenye najisi kwa kutumia kata au bomba la maji.
(2) Sugua au suka-suka sehemu yenye najisi.
(3) Mimina maji yapitie sehemu yenye najisi mpaka rangi na harufu viondoke.
(4) Unaweza kutumia sabuni ili kuondoa harufu na rangi kwa urahisi.



Book3.indb 48 4/19/05 7:04:32 AM



**Tahadhari**

(1) Usitumbukize nguo yenye najisi ndani ya ndoo, kwani maji yote kwenye ndoo yatanajisika.
(2) Wakati wa kutoa najisi jihadhari na cheche za maji yenye najisi zisikurukie mwilini au kwenye nguo ulizovaa.
(3) Ni vizuri wakati wa kuondoa najisi uchuchumae ili maji yasiruke.

**Kuondosha najisi kubwa**

Najisi kubwa huondoshwa kwa maji safi na udogo safi kwa makosho saba. Mtume Muhammad (s.a.w) ametuagiza:

> *"Kutwaharisha kwa chombo cha yoyote kati yenu baada ya kulambwa na mbwa ni kukiosha mara saba, ukitumia udongo katika safari ya kwanza."*

Hivyo najisi kubwa huondoshwa kama ifuatavyo:

(1) Safisha sehemu iliyoingia najisi mpaka rangi na harufu viondoke.
(2) Sugua sehemu iliyokuwa na najisi kwa udongo safi.
(3) Kisha ioshe sehemu hiyo kwa makosho sita ya maji.



Book3.indb 49 4/19/05 7:04:34 AM

Udongo hutumika ili kuua ijidudu vibaya vitokanavyo na mbwa na nguruwe.

**Maji safi**
Maji safi yanayotumika kwa ajili ya kutia udhu au kuondoshea najisi ni yale yaliyo katika asilia (natural water). Maji ya asili ni:

(1) Maji ya mvua.
(2) Maji ya bahari.
(3) Maji ya mto.
(4) theluji/barafu.
(5) Maji ya ziwa.
(6) Maji ya kisima.

**Maji machache**
Maji yaliyotekwa kwenye chombo kidogo kama vile ndoo au beseni ni maji machache. Maji haya hayafai kutawadhia au kuondolea najisi iwapo:

(1) Yameingiwa na najisi japo kidogo.
(2) Yamebadilika rangi ya sili.
(3) Yamebadilika harufu yake ya asili.
(4) Yamebadilika utamu wake wa asili.
(5) Yamesuuziwa nguo au vyombo.
(6) Yametumika kwa kutawadhia au kunawia humo humo.

Wakati wa tukitumia maji machache hatunabudi kutumia kata na kutawadhia pembeni.

**Maji ya kulatain (Maji mengi).**
Maji ya kulatain ni maji mengi yenye ujazo wa debe 12 au zaidi. Maji ya hodhi, maji ya mabwawani ni maji mengi. Maji mengi hayaharibiki upesi. Hayaharibiki kwa kunawia humo au kutawadhia humo. Hata yakiingiwa na najisi, bado yanafaa kutawadhia au kuondoshea najisi. Maji ya kulatain huharibika kwa

(1) Kubadilika rangi yake ya asili.
(2) Kubadilika harufu yake ya asili.
(3) Kubadilika utamu wake wa asili.

**Maji makombo**


Book3.indb 50 4/19/05 7:04:35 AM

Maji makombo ni maji yaliyonywewa na kubaki. Maji yaliyonywewa na mtu yakabaki ni maji safi. Maji yaliyonywewa na mnyama yakabaki ni maji safi ila mnyama huyo asiwe mbwa wala nguruwe.

**Sharti za udhu**

Kabla hujaanza kutia udhu hunabudi kuzingatia shuruti zifuatazo:

(1) Kuwa na maji safi ya kutosha kutiririka kwenye viungo vya udhu (angalau yawe lita moja).

(2) Pasiwe na kitu kilichogandamana katika viungo vya udhu – uso, mikono mpaka vifundoni na miguu mpaka vifundoni. Vitu vinavyogandamana ni kama lami, rangi, bigijii, nta, na kadhalika.

(3) Pasiwe na vumbi au matope kwenye viungo vya udhu. Kwa mfano pasiwe na vumbi la mkaa, unga au vumbi la udongo.

(4) Pasiwe na najisi katika viungo vya udhu.

(5) Pasiwe na makucha marefu yanayozuilia maji kupenyeza ndani kwenye ncha za vidole.

**Kutia udhu**

Allah (s.w) ametuamrisha kutia udhu kama ifuatavyo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِذَا قُمْتُمْ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ فَٱغْسِلُوا۟
وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى ٱلْمَرَافِقِ وَٱمْسَحُوا۟ بِرُءُوسِكُمْ

*"Enyi mlioamini mnaposimama ili mkaswali basi osheni nyuso zenu mikono yenu mpaka vifundoni na mpake vichwa vyenu na osheni miguu nyenu mpaka vifundoni…" (5:6).*

Allah (s.w) na Mtume wake wametuamrisha tutie udhu kama ifuatavyo:

(1) Kutia nia moyoni (kuwa tunatawadha).

(2) Kuosha uso kwa mipaka yake.

(3) Kuosha mikono mpaka vifundoni ukianza na mkono wa kulia.

(4) Kupaka maji kichwani.

(5) Kuosha miguu mpaka vifundoni ukianza na wa kulia.



Book3.indb 51 4/19/05 7:04:42 AM

(6) Kufuatisha utaratibu huu.

**Namna Mtume (s.a.w) alivyotia udhu**

Mtume (s.a.w) alitia udhu kama ifuatavyo:

(1) Alipiga mswaki kabla hajaanza kutia udhu.

(2) Alitia nia na kuanza kwa Bismillahir Rahmaanir Rahiim.

(3) Aliosha vitanga vya mikono mara tatu.

(4) Alisukutua na kupandiliza maji puani mara tatu.

(5) Aliosha uso mara tatu.

(6) Aliosha mikono mpaka vifundoni akianza na kulia mara tatu.

(7) Alipaka maji kichwani kuanzia mbele kwa viganja vya mikono miwili mpaka nyuma mara tatu.

(8) Alipaka masikio maji kwa kutia kidole cha shahada ndani na kupitisha kidole gumba nyuma ya sikio mara tatu.

(9) Aliosha miguu miwili mpaka vifundoni akianzia kulia mara tatu.

Hatunabudi kutawadha kama Mtume alivyotawadha. Tunatakiwa tumuige Mtume kwa kila kitu. Baada ya kutia udhu Mtume (s.a.w) ametufundisha dua ifuatayo:-

اَللَّهُمَّ إجْعَلْنِي مِنَ تَوَّابِينَ وَاجْعَلْنِي
مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ وَاجْعَلْنِي مِنْ عِبَادِكَ
الصَّالِحِينَ

*na unijaalie niwe miongoni mwa wenye kutakasika na unijaalie niwe miongoni mwa wenye kutakasika na unijaalie niwe miongoni mwa waja wako wema".*



Book3.indb 52 4/19/05 7:04:44 AM

**Kutoka na Udhu**

Mtu hutokwa na udhu kwa:

(1) Kwenda haja ndogo au kubwa.
(2) Kutokwa na kitu chochote katika utupu wa mbele au nyuma.
(3) Kutokwa na upepo nyuma.
(4) Kushika tupu ya mbele au ya nyuma kwa matubo viganja vya mikono.
(5) Kulala usingizi au kuzimia.
(6) Kurukwa na akili.


Kusinzia huku umekalisha makalio yako vizuri ardhini hakutengui udhu.


**Sitara katika swala**

Muislamu anatakiwa ajisitiri vizuri muda wote. Avae nguo zinazokubalika kiislamu kwa kujisitiri vizuri wakati wote na kila anapokwenda kuswali.

**Mipaka ya sitara kwa wanaume**

Mipaka ya sitara kwa mwanaume ni kufunika sehemu yote iliyo kati ya kitovu na magoti. Kitovu na magoti na sehemu iliyobaina yake ifichwe. Katika dharura mwanaume anaweza kuswali na kikoi tu bila shati.





Katikati hali ya kawaida ni vema kuvaa vizuri wakati wa kwenda kuswali kama Allah anavyotuamrisha.



Book3.indb 53 4/19/05 7:04:46 AM

يَٰبَنِيٓ ءَادَمَ خُذُواْ زِينَتَكُمۡ عِندَ كُلِّ مَسۡجِدٖ

*"Enyi wanaadamu! Chukueni mapambo nyenu wakati wa kila swala. (7:31).*

**Mipaka ya sitara kwa wanawake**

Sitara ya mwanamke wa Kiislamu hupatikana kwa kufunika mwili mzima isipokuwa uso na vitanga vya mikono na kushusha shungi mpaka kifuani.



Mwanamke wa Kiislamu anatakiwa ajisitiri wakati wote kama anavyojisitiri akiwa katika swala.

**Kuswali kwa wakati**

Swala tano zimeamrishwa ziswaliwe kwa wakati maalum:

إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتۡ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ كِتَٰبٗا مَّوۡقُوتٗا ١٠٣

*"Kwa hakika swala kwa waumini ni faradhi iliyowekewa nyakati makhsusi.(Qur-an, 4:103).*



Book3.indb 54 4/19/05 7:04:53 AM

Nyakati za swala zinafuata mwenendo wa jua. Ratiba za swala zimebandikwa katika misikiti mbali mbali. Kwa wastani nyakati za mwanzo wa swala kwa wakazi wa Dar es Salaam (kanda ya mashariki ya Tanzania) ni:

### NYAKATI ZA SWALA TANO ZA FARADHI

| | Swala | Wakati | Majira |
|---|---|---|---|
| 1. | **Subuhi** | **11:15** | **Alfajiri** |
| 2. | **Adhuhuri** | **6:45** | **Adhuhuri** |
| 3. | **Alasiri** | **9:45** | **Alasiri** |
| 4. | **Magharibi** | **12:30** | **Magharibi** |
| 5. | **Al-Isha** | **1:45** | **Usiku** |

Kila swala inatakiwa iswaliwe kwa wakati wake. Kila swala iswaliwe kabla ya wakati wa swala inayofuatia kuingia. Swala nje ya wakati wake haikubaliki. Muislamu akiwa kazini, shambani au shuleni, hanabudi kufanya utaratibu wa swala huko huko hata kama hakuna msikiti karibu. Popote pale panafaa kuswalia, ila tu pasiwe na najisi.

**Kuelekea Qibla**

Tunalazimika kuelekea Qibla wakati wa kuswali. Qibla cha Waislamu wa ulimwengu wote ni Ka'aba. Ka'aba ni nyumba takatifu ya Allah iliyopo ndani ya msikiti wa Makka, nchini Saudi Arabia. Hivyo, tukiswali tunaelekea ilipo Ka'aba.

Amri ya kuelekea Ka'aba kila tunapo swali ipo katika Qur-an. Allah (s.w) anatuamrisha kwa kusema:



Book3.indb 55 4/19/05 7:04:54 AM

وَحَيْثُ مَا كُنتُمْ فَوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُۥ

*"Na popote mlipo geuzeni nyuso zenu upande iliko Ka'abah (2:150).*

**Nguzo za Swala**

Katika kitabu cha pili tumejifunza namna ya kuswali kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Ili swala ikamilike hatunabudi kutekeleza nguzo za swala zifuatazo:

1. Kutia nia moyoni.
2. Kuanza swala kwa Takbira ya kuhirimia.
3. Kusoma Suratul-Fatiha (Al-hamdu).
4. Kurukuu (kuinama).
5. Kujituliza katika Rukuu.
6. Kuitidali (kusimama kutoka rukuu).
7. Kujituliza kwenye itidali.
8. Kusujudu sijda ya kwanza.
9. Kujituliza kwenye Sijda.
10. Kukaa kati ya sijda mbili.
11. Kujituliza katika kikao cha katika sijda mbili.
12. Kusujudu sijda ya pili.
13. Kujituliza kwenye sijda ya pili.
14. Kukaa tahiyyatu.
15. Kusoma tahiyyatu.
16. Kumswalia mtume.
17. Kutoa Salaam.

**Rakaa**

Rakaa moja hupatikana kwa kutekeleza vitendo vyote kuanzia kitendo cha 1 hadi 13 kwa kufuata utaratibu huo. Kila baada ya rakaa mbili kuna kukaa tahiyatu. Swala zenye rakaa zaidi ya mbili zina tahiyyatu mbili. Kukaa tahiyyatu ya pili ni nguzo ya 14.



Book3.indb 56 4/19/05 7:05:02 AM

## IDADI YA RAKAA NA TAHIYYATU KATIKA SWALA

| | SWALA | RAKAA | RAHIYYATU |
|---|---|---|---|
| 1 | Subuhi | 2 | 1 |
| 2 | Dhuhuri | 4 | 2 |
| 3 | Al-asiri | 4 | 2 |
| 4 | Magharibi | 3 | 2 |
| 5 | Ishaa | 4 | 2 |
| | Jumla | 17 | 9 |

**Baadhi ya Sunnah za Swala**
1.Kuinua mikono

Kuinua mikono katika swala ni sunna. Mtume (s.a.w) alipokuwa akiswali aliinua mikono wakati wa:

- Kuhirimia swala.
- Akitoka kwenye rukuu (akiitidali).
- Akisimama kutoka kwenye sijida ya pili.

Tumuigize Mtume (s.a.w). tuinue mikono kama alivyoinua. Aliinua viganja vyake vya mikono mkabala na mabega vidole gumba vikiwa usawa wa masikio






Book3.indb 57 4/19/05 7:05:03 AM

2.Dua baada ya Takbira ya kuhirimia. Ni sunna baada ya kuhirimia swala kusoma dua ifuatayo:

Dua baada ya Takbira

وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِيْ فَطَرَالسَّمَاوٰتِ وَالأَرْضَ

*"Nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi.*

حَنِيْفًا وَمَآ اَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ

*Nimeacha dini za upotovu. Na Mimi si miongoni mwa Washirikina.*

اِنَّ صَلاَتِىْ وَنُسُكِيْ وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِىْ لِلّٰهِ

رَبِّ ٱلْعلَمِينَ

*Hakika swala yangu, na Ibada zangu zote ni kwa ajili ya Allah, Bwana wa walimwengu wote.*

لاَشَرِيْكَلَهُ وَبِذَالِكَ اُمِرْتُ وَ اَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ

*Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyoamrishwa na mimi ni miongoni mwa waliojisalimisha kwa Allah".*

Dua hii husomwa kabla ya kuanza kusoma Al-Hamdu (Suratul-Fatiha).

4.Dua kabla ya kutoa salaam

Baada ya kumswalia Mtume na kabla ya kutoa Assalaam ni vema kusoma dua ifuatayo:

اَللَّهُمَّ اِنِّىْ ظَلَمْتُ نَفْسِىْ ظُلْمًا كَبِيرًا

*Ee Allah! Hakika nimedhulumu nafsi yangu dhulma kubwa.*



Book3.indb 58 4/19/05 7:05:06 AM

وَلاَيَغْفِرُ الذُّنُوْبَ اِلاَّ أَنْتَ

*Hapana yeyote mwenye kusamehe dhambi siipokuwa wewe tu.*

فَاغْفِرْلِى مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ

*Basi nakuomba unipatie msamaha utokao kwako na unihurumie.*

وَرْحَمْنِى، إِنَّكَ أَنْتَ الغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ

*Hakika wewe ni msamehevu mwenye huruma."*

**Yanayobatilisha swala**

Wakati wa kuswali Muislamu anatakiwa awe mtulivu na Mnyenyekevu kwa Allah. Muislamu akiswali huwa anaongea na Allah. Ajichunge na yale yanayobatilisha swala.

**Yafuatayo yanabatilisha swala**

(1)Kutoelekea qibla makusudi.

(2)Kuvukwa na nguo na kubaki uchi.

(3)Kutengukwa na udhu.

(4)Kuingiwa na najisi.

(5)Kula au kunywa ndani ya swala.

(6)Kuzungumza ndani ya swala.

(7)Kucheza cheza ndani ya swala.

(8)Kulala ndani ya swala.

(9)Kuacha nguzo ya swala.

(10)Kufanya kitendo kilicho nje ya vitendo vya swala.

(11)Kutia nia ya kuvunja swala.



Book3.indb 59 4/19/05 7:05:07 AM



## Zoezi la Tatu

1. (a) Uislamu maana yake ni.............................................................................
   (b)Taja nguzo tano za Uislamu kwa mtiririko kuanzia nguzo ya kwanza

2. (a) Mtu anaposilimu hutamka............ambayo maana yake ni.......................
   (b) Taja tabia njema kumi

3. Ni ipi tofauti iliyopo baina ya muislamu na mnafiki

4. (a) Najsi ni .......................................
   (b) Taja aina tano za najsi unazozijua
   (c)Ni ipi tofauti ya Najsi kubwa na Najsi ndogo

5. Eleza namna utakavyoondosha najsi kubwa hatua kwa hatua.

6. (a) Onesha tofauti baina ya maji mengi na maji machache
   (b) Onesha kwa vitendo namna Mtume (s.a.w) alivyokutia udhu.

7. Sitara ya mwanamke ni......................... isipokuwa............... na................

8. Sitara ya mwanaume ni...........................................................................

9. Muislamu anapotaka kuswali ni lazima aelekee...........................................

10. Tia udhu kisha uswali swalatu dhuhri

11. Ni mambo yepi yanayobatilisha swala?



Book3.indb 60 4/19/05 7:05:08 AM

## Somo la 4. Akhlaq

# USAFI NA UNADHIFU

**Usafi**

Uislamu ni dini ya usafi na unadhifu.Uislamu unasisitiza usafi na unadhifu wa mwili, nguo, mazingira na usafi wa tabia. Allah (s.w) anatuamrisha waislamu kuwa watu safi na nadhifu katika aya zifuatazo:

وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾ وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ ﴿٥﴾ وَلَا تَمْنُن تَسْتَكْثِرُ ﴿٦﴾
وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ﴿٧﴾

*Na nguo zako uzitakase, na maovu uyaepuke na wala usifanye wema kwa kutaka umaarufu.(74:3-6)*

Naye Mtume Muhammad(s.a.w) katika kusisitiza usafi amesema:

*"Uislamu ni nadhifu, basi jinadhifisheni."*

**Unadhifu wa mwili**

Ili Muislamu awe na mwili nadhifu hanabudi kujitahidi kufanya yafuatayo:

**(i) Kupiga mswaki kila mara**

Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa na kawaida ya kupiga mswaki mara kwa mara. Alipiga mswaki kila alipoamka kutoka usingizini, baada ya kula na kabla ya kutia udhu. Hatunabudi kumfanya Mtume (s.a.w) kuwa kiigizo chetu katika jambo hili.



Kuhusu suala la kupiga mswaki, Mtume (s.a.w) mwenyewe anatuhimiza katika hadithi zifuatazo:-



Book3.indb 61 4/19/05 7:05:12 AM



*Aisha (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema:"Mswaki unatakasa mdomo na ni njia ya kupatia radhi za Allah (s.w). (Bukhari).*

*"Abu-Hurairah (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema, "Isingelikuwa kwamba nitawapa mzigo ningeliwaamrisha (Waislamu) wapige mswaki kila wanapotawadha." (Bukhari).*

Faida za kupiga mswaki mara kwa mara ziko wazi:

(i) Huufanya mdomo kuwa safi na kuepukana na harufu mbaya.
(ii) Huyafanya meno kuwa safi.
(iii) Huyahifadhi meno kutokana na magonjwa mbali mbali.
(iv) Humpelekea Muislamu kupata radhi za Allah (s.w).

**(ii) Kuwa na nywele nadhifu**

Muislamu anatakiwa kila mara ahakikishe kuwa nywele zake ni nadhifu. Ni sunnah kwa mwanaume kuwa na nywele fupi. Kila wakati nywele za kijana wa Kiislamu ziwe zinaoshwa na kusuguliwa vizuri kila anapooga na zichanwe vizuri kila mara. Kijana wa Kiislamu aepukane na kunyoa mitindo ya kihuni kama vile "*Panki*" na kadhalika.

Ni Sunnah kwa muislamu mwanamke kuwa na mwele ndefu zilizochanwa vizuri na kubakia katika asili yake. Wanawake wa Kiislamu wanaruhusiwa kusuka nywele zao kwa mitindo mbali mbali ila tu usiwe ule wa kuweka nywele za bandia kichwani.

Ni haramu kwa Muislamu kubadilisha nywele kwa madawa, kuvaa nywele za bandia, kuunganisha nywele, kusuka mtindo wa Rasta, n.k.

**(iii) Kuwa na kucha nadhifu**

Muislamu anatakiwa akate kucha zake kila zinaporefuka, angalau akate kucha za miguuni na mikononi kila wiki mara moja. Kucha ndefu huweka uchafu na ni hatari kwa afya. Vile vile kucha ndefu huzuia maji kupenyeza kwenye ncha za vidole wakati wa kutawadha au kukoga josho la wajibu.

Waislamu haturuhusiwi kupaka rangi kwenye kucha. Rangi huzuia maji


Book3.indb 62 4/19/05 7:05:14 AM

kupenyeza wakati wa kutawadha au kukoga josho la wajibu. Hivyo mwenye kupaka-paka rangi hawezi kuwa twahara. Mtu asiye twahara hawezi kusimamisha swala. Asiyesimamisha swala si Muislamu kwa mijibu wa Qur-an na Hadith sahihi za Mtume (s.a.w).

**(iv) Kujinadhifisha mwili mzima**

Muislamu anawajibika kuwa na mwili nadhifu kila mara. Mtoto wa Kiislamu hanabudi kukoga kila siku kabla ya kaulala, baada ya harakati za mchana kutwa. Ni vizuri kukoga kwa sabuni na kujisugua kwa dodoki au kwa nyuzinyuzi za manila au mkonge.

Mahali pa kukogea pawe faragha. Kama unakogea bafuni, ufunge mlango au ushushe pazia. Ni haramu Muislamu kudhihirisha uchi wake kwa mtu mwingine. Hivyo ni haramu kukoga mawili katika bafu moja. Kama unakogoea mtoni, basi tafuta mahali paj faragha.

Unadhifu wa mwili haupatikani kwa kukoga tu bali pamoja na kujizuilia na kufikwa na najisi hasa wakati wa kwenda haja kubwa au ndogo. Muislamu hanabidi kustanji vizuri baada ya kwenda haja.

**Unadhifu wa nguo**

Unadhifu wa mwili hautatengemaa iwapo nguo zitakuwa chafu. Mtoto wa Kiislamu hana budi kuvaa nguo safi na kujiepusha na hali ya kujichafua ovyo ovyo. Mtoto wa darasa la tatu ana uwezo wa kufua nguo zake vizuri na kuzipiga pasi.









Book3.indb 63 4/19/05 7:05:16 AM

**Unadhifu wa mazingira**
Mazingira ya nje ya nyumba ya Muislamu yanatakiwa yawe safi. Kama kuna wasaa wa eneo, pawe na bustani za maua za kuzunguka nyumba, pawe na barabara na viwanja. Eneo lote liwe safi na pawe na shimo la takataka zichomwe moto taka zinazochomeka.



Usafi wa mazingira hapa unazingatia usafi wa ndani na nje ya nyumba.


**(i) Usafi wa ndani ya nyumba**
Kwa ujumla nyumba ya Muislamu hainabudi kuwa safi na vitu ndani yake kuwa katika mpangilio mzuri. Nyumba haina budi kufagiliwa na kupigwa deki kila siku iwapo imesakafiwa kwa saruji. Kama haijasakafiwa inyunyiziwe maji kila siku ili pasiwe na mavumbi. Angalau mara moja kwa wiki pawe na kawaida ya kutandua mabuibui, kufuta vumbi madirishani, milangoni, ukutani na kadhalika.

Ili kuhakikisha mazingira ya ndani ya nyumba yanakuwa nadhifu katika kiwango kinachoridhisha, tuangalie kwa undani sehemu muhimu kama sebuleni, chumbani, jikoni na chooni au bafuni.

**Sebuleni**
Sebuleni ni ukumbi wa kupokelea wageni na sehemu ya kukutana pamoja wakazi wa nyumba. Hapanabudi kuwa mahali pa kupendeza, viti, meza, sofa, vitambaa, maua na kadhalika, viwe katika mpango mzuri. Sebuleni au sehmu nyingine yoyote ya nyumba isiwe na masanamu ya watu au wanyama wala pasiwe na picha za watu zilizobandikwa ukutani au zilizoegeshwa mahali popote pale. Kwani nyumba yenye vitu hivyo haifikiwi na malaika wa kheria kwa mujibu na Hadithi ifuatayo:



Book3.indb 64 4/19/05 7:05:17 AM



*Abu Talha (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema "Malaika hawaingii nyumba yenye mbwa na picha". (Bukhari na Muslim).*

Pia nyumba ya Muislamu haipaswi kuwa na picha yoyote ya msalaba.

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) hakuweka kitu chochote nyumbani kwake chenye picha ya msalaba bila ya kukiharibu. (Bukhari).*

Mara nyingi sebuleni huwekwa radio, T.V, radio na T.V. ni vyombo vizuri vya habari na taaluma iwapo vitatumiwa kwa madhumuni hayo tu. Vinginevyo programu nyingi za vyombo vya habari zimewekwa kwa ajili ya kufisidi maadili ya Kiislamu. Kuna michezo, miziki, sinema na vichekesho vilivyowekwa kwa lengo la kuwapumbaza watu, hasa wototo na vijana ili kuwavua maadili ya Kiislamu na kuwavisha badala yake maadili ya kishetani. Michezo yote ile inayopoteza muda na kupalilia maaadili ya kishetani katika Qur-an imeitwa Laghwi na imeharamishwa kwa Waislamu. Waislamu wa kweli ni wote wanaojiepusha na *Lagh-wi* kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ ﴿٢﴾
وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

*"Hakika wamefuzu waumini ambao katika swala zao huwa wenyenyekevu ambao hujiepusha na lagh-wi (mambo ya upuuzi). (23:1-3).*




Book3.indb 65 4/19/05 7:05:26 AM

Hivyo Waislamu tunatakiwa tuwe waangalifu katika kutumia radio na T.V. Hatunabudi kuzima radio au T.V. mara tu baada ya taarifa za habari au vipindi vya mafundisho mazuri kwisha. Tusipafanyue sebuleni petu kuwa ukumbi wa mambo ya kishetani kama Disko au Sinema za hovyo.


**Chumbani**

Chumba anacholala Muislamu kiwe nadhifu. Kiwe kinasafishwa vizuri. Kitanda kiwe kimetandikw avizuri kwa shuka safi. Viti, kabati, meza, na kadhalika, viwekwe kwenye mpangilio mzuri.



**Jikoni**

Jikoni pawe safi. Vyombo visafishwe vizuri kwa sabuni na brashi mara tu baada ya kutumika. Baada ya kusafishwa, vyombo vikaushwe kwa vitambaa safi na kufunikizwa ndani ya kabati au juu ya meza au kichanja cha vyombo.





Book3.indb 66 4/19/05 7:05:27 AM


Mtungi au pipa au chombo kingine chochote cha kuhifadhia maji kiwe na mfuniko. Mtume (s.a.w) amehimiza kufunika maji katika hadithi ifuatayo:-


> *"Jabir bin 'Abdullah (r.a) ameeleza kuwa alimsikia Mtume wa Allah akisema, 'Funika Mtungi na funga kwa kamba mfuniko' (Muslim).*

Jiko lazima lizimwe mara baada ya kupika ili kujihadhari na kuunguza nyumba, kutumia ovyo mkaa au mafuta au umeme au kuni.

**Chooni na Bafuni**

Kila nyumba ya Muislamu ni lazima iwe na choo na bafu. Usafi wa hali ya juu unahitajika chooni na bafuni. Kila mara pasafishwe na kupigwa deki. Kama kinatumika choo cha maji ya kuvuta, beseni la choo liwe safi nyakati zote. Maji mengi yatumiwe kusukuma uchafu mara baada ya kumaliza haja. Pawe na brashi ya kusafishia iliyo tayari-tayari.





Kama kinatumika choo cha shimo, tundu la choo lifunikwe kwa mfuniko uliotengenezwa kwa ubao au bati.



Book3.indb 67 4/19/05 7:05:29 AM

**Kumkumbuka Allah muda wote**

Lengo la maisha ya mwanaadamu hapa ulimwenguni ni kumuabudu Allah (s.w) kama tunavyofahamishwa na Qur-an:

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ٥٦

*"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu". (51:56).*

Kumuabudu Allah (s.w) kama lengo la maisha ya kumtii Allah (s.w) na Mtume wake katika maisha yetu yote. Ni kufuata yale yote aliyotuamrisha Allah (s.w) na Mtume wake na kuacha yale yote waliyotukataza katika maisha yetu yote. Tutaweza kumuabudu Allah (s.w) katika kila pumzi ya maisha yetu iwapo tutafanya kila jambo kwa kuchunga mipaka ya Allah (s.w) na kufuata sunnah ya Mtume (s.a.w), kwa mfano:

- Tukila chakula halali na kuzingatia adabu za kula kama alivyotufundisha mtume (s.a.w) tutakuwa tunamuabudu Allah (s.w).
- Tukifanya kazi kwa bidii ili kuwasaidia wazazi wetu tutakuwa tunafanya Ibada kwa kuwa tunafuata agizo la Allah (s.w).
- Tukisalimiana kwa salamu ya Kiislamu tutakuwa tunamuabudu Allah (s.w). Kwani yeye ndiye aliyetufundisha na kutuelekeza tutumie salamu hiyo.
- Tukicheza ili tuwe na siha nzuri, tuwe wachangamfu na wakakamavu tutakuwa tunamuabudu Allah (s.w) ili mradi tu tuchunge mipaka ya Allah na Mtume wake wakati wa kucheza.

Nyezo muhimu zitakazotuwezesha kumuabudu Allah katika kila jambo letu tunalolifanya ni:

(1) Kuanza kila jambo jema kwa Bismillahir Rahmaanir Rahiim.

(2) Kusimamisha swala tano ipasavyo. Kwani Allah (s.w) anatufahamisha:



Book3.indb 68 4/19/05 7:05:33 AM

إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ

*Bila shaka swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuilia (mtu kufanya) mambo machafu na maovu…" (29:45).*

(3) Kufunga ramadhani na funga nyingine za Sunnah kama vile funga ya Jumatatu na alhamis, funga ya Ashura na funga ya Arafa.

(4) Kutoa Zakat na Sadaqat na kuhiji makka kwa mwenye uwezo.

(5) Kufanya kila jambo jema kwa kumuigiza Mtume na kuleta dua aliyotufudisha kwa mfano:

- Tukiamka kutoka usingizini alfajiri au wakati mwingine tutasema:

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِى اَحْيَانَا بَعْدَ مَا اَمَاتَنَا
وَاِلَيْهِ النُّشُوْرُ

*Shukrani zote ni za Allah (s.w) ambaye ameturejesha katika uhai baada ya kutufisha. Na yeye ndiye atakayafufua." (Bukhari na Muslim).*

- Tukienda haja tutangulize mguu wa kushoto chooni kisha tuseme:

اَللّٰهُمَّ اِنِّى اَعُوْذُبِكَ مِنَ الْخُبْثِ وَالْخَبَائِثِ

*Ee! Allah najikinga kwako na uchafu na uovu wa aina zote.*



Book3.indb 69 4/19/05 7:05:38 AM

- Tukimaliza haja, tutoke chooni kwa kutanguliza mguu wa kulia na kusema:

اَلحَمْدُلِلّٰهِ الَّذِى اَذْهَبَ عَنِّى الأَذَى وَعَافَانِى

*"Sifa zote (shukrani zote) anastahiki Allah ambaye ameniondolea uchafu na kunipa Afya."*

- Tukivaa nguo tuanze kuvaa mkono au mguu wa kulia na tusome:

اَلحَمْدُلِلّٰهِ الَّذِى كَسَانِى هَذَا وَرَزَقَنِيهِ

غَيْرِ حَوْلٍ مِنِّى وَلَاقُوَّةٍ

*Shukrani zote anastahiki Allah (s.w) aliyenivisha vazi hili na aliyeniruzuku bila kuwa na uwezo au nguvu yoyote.*

- Tukitoka nyumbani tumwachie Allah (s.w) ulinzi wa nyumba zetu kwa kusema:

بِسْمِ اللّٰهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللّٰهِ وَلَا حَوْلَ وَلَاقُوَّةَ اِلَّا بِاللّٰهِ

*"Kwa jina la Allah, Ninajitegemeza kwa Allah, hapana uwezo au nguvu ila kutoka kwa Allah".*

- Tukirejea nyumbani tuseme kama alivyokuwa akisema Mtume (s.a.w):

اَللَّهُمَّ اِنِّى اَسْئَلُكَ خَيْرَالمَوْلِجِ وَخَيْرَالمَخْرَجَ



Book3.indb 70 4/19/05 7:05:40 AM

*"Ee Allah nakuomba unipe uhai kutokana na kuingia kwangu na kutoka kwangu.*

- Tukiingi msikitini tunatanguliza mguu wa kulia na kusema:

اَعُوْذُ بِاللهِ الْعَظِيْمِ وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيْمِ وَسُلْطَانِهِ
الْقَدِيْمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ

*"Na jikinga kwa Allah aliyetukuka na kwa Wajihi wake mtukufu na kwa uweza wa utawala wake kutokana na shaitwani aliyelaaniwa".*

Au tusema:

بِسْمِ اللهِ وَالصَّلاَةُ وَالسَّلاَمُ عَلَى رَسُوْلِ اللهِ،
رَبِّ اغْفِرْلِى ذُنُوْبِى وَافْتَحْلِى اَبْوَابَ رَحْمَتِكَ

*"Kwa jina la Allah, Rehma na amani zimwendee Mtume wa Allah, Ee Bwana Mlezi (ee Mola) Nisamehe madhambi yangu na nifungulie milango ya rehma yako.*

- Tukitoka msikitini tutangulize mguu wa kushoto tuseme:

اَللَّهُمَّ اِنِّى اَسْئَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ

*Ee Allah nakuomba unifungulie milango ya fadhila zako.*



Book3.indb 71 4/19/05 7:05:42 AM

Au tusema:

بِسْمِ اللهِ وَالصَّلاَةُ وَالسَّلاَمُ عَلَى رَسُوْلِ اللهِ ، رَبِّ اغْفِرْلِي ذُنُوبِي وَافْتَحْلِي أَبْوَابَ فَضْلِكَ

*"Kwa jina la Allah, Rehma na Amani zimuendee Mtume wa Allah, Ee Mola wangu, nisamehe madhambi yangu na nifungulie milango ya fadhila zako".*

- Tuwasalimie waislamu wenzetu kwa kusema:

اَلسَّلاَمُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ

*"Amani iwe juu yenu na rehma za Allah na Baraka zake.*

- Tunaposafiri na gari au ndege au meli au kipando kingine chochote, tuanze kuapanda kwa mguu wa kulia kwa kusema:

*Bismillah* بِسْمِ اللهِ

Kisha tukikaa tuseme: اَلحَمْدُ لِلهِ

*"Shukrani zote anastahiki Allah".*

Kisha tusema:

سُبْحَانَ الَّذِيْ سَخَّرَلَنَا هَاذَا وَمَاكُنَّالَهُ مُقْرِنِينَ وَاِنَّآ اِلَى رَبِّنَا لَمُ نْقَلِبُوْنَ



Book3.indb 72 4/19/05 7:05:45 AM

*"Utukufu ni wa yule aliyetutiishia kipando hiki ambacho hatuna uwezo wa kukitenza nguvu, Hakika kwa Mola wetu ndio marejeo yetu".*

- Tukipiga chafya tusema:

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ

*"Shukrani zote anastahiki Allah:*

Kisha wengine waitikie:

يَرْحَمُكَ اللّٰهُ

*Mwenyezi Mungu akurehemuni.*

Kisha aliyepiga chafya aendelee kusema:

يَهْدِيْكُمُ اللّٰهُ وَيُصْلِحُ بَالَكُمْ

*"Allah akuongozeni na akusahilishieni mambo yenu".*

- Tuwatembelee wagonjwa na tuwasomee mara saba dua ifuatayo:

اَسْئَلُكَ اللّٰهَ الْعَظِيمَ رَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ

اَنْ يَّشْفِيكَ

*"Namuomba Allah aliyemtukufu, bwana wa Arsh tukufu akuponyeshe". (mara saba 7)*



Book3.indb 73 4/19/05 7:05:46 AM

Pia Mtume (s.a.w) alipougua yeye mwenyewe au watu wake wa nyumbani walipougua alisoma sura mbili za kujikinga – suratul-Falaq na An-Naas. Kisha alikuwa akijipuliza au kuwapuliza watu wake. Nasi tumuigize mtume (s.a.w). Kwa kujifanyia sisi wenyewe na tunapowatembelea wagonjwa wetu.

- Tunapopita kwenye makaburi ya Waislam

اَلسَّلاَمُ عَلَيْكُمْ اَهْلَ الدِّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ
وَالْمُسْلِمِينَ وَ إِنَّآ اِنْشَآءَاللّٰهُ بِكُمْ لاَحِقُوْنَ
نَسْئَلُ اللّٰهَ لَنَا وَلَكُمُ العَافِيَةَ

*"Amani iwe juu yenu Enyi wakazi wa hapa miongoni mwa waumini wa waislamu, Allah akipenda tutakutana. Tunamuomba Allah atupe afya pamoja nanyi.*

- Tuombe msamaha kwa Allah kila mara kwa kusema:

اَسْتَغْفِرُاللّٰهَ

*"Naomba msamaha kwa Allah"*

Pia ni vizuri mara kwa mara kuomba maghfira kwa kusema:

رَبَّنَآ اِنَّنَآ اٰمَنَّآ فَغْفِرْلَنَا ذُنُوْبَنَا وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

*"… Mola wetu! Hakika sisi tumeamini basi tughufirie madhambi yetu na tuepushe na adhabu ya moto". (3:16)*

- Wakati wa kulala tunalalia ubavu wa kulia na kusema:

اَللَّهُمَّ بِاسْمِكَ اَمُوْتُ وَاَحْيَا



Book3.indb 74 4/19/05 7:05:48 AM

*"Ee Allah, kwa jina lako, ninakufa na kuhuika".*

**5. Kumkumbuka Allah (s.w) wakati wa Ukimya:**

Muislamu hana muda wa kupoteza. Kama hana shughuli yoyote ya kufanya anatakiwa amkumbuke Allah (s.w) kwa kuleta dhikri zifuatazo:

سُبْحَانَ اللّٰهَ وَبِحَمْدِهِ سُبْحَانَ اللّٰهَ الْعَظِيمِ

*"Utukufu ni wa Allah na sifa zote zinamstahiki yeye, utukufu ni wa Allah aliye mkuu.*

Mtume (s.a.w) anasema maneno haya ni mepesi katika ulimi lakini ni mazito katika mizani.

سُبْحَانَ اللّٰهَ، وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ، وَلَآ اِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ، وَاللّٰهُ أَكْبَرُ

*"Utukufu ni wa Allah, sifa zote anastahiki Allah, hapana Mola ila Allah na Allah ni Mkubwa".*

Mtume (s.a.w) anasema kutamka maneno haya kwa dhati na kwa mazingatio ni bora mbele ya Allah kuliko kitu chochote kinachoangaziwa na jua.

سُبْحَانَ اللّٰهَ وَبِحَمْدِهِ عَدَدَ خَلْقِهِ وَرِضَا نَفْسِهِ وَزِنَةَ عَرْشِهِ وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ

*"Utukufu ni wa Allah na sifa zote zinamstahikia yeye kwa idadi ya viumbe vyake vyote, kwa kiasi cha ridhaa ya nafsi yake kwa kiasi cha uzito wa arshi yake na kwa kiasi cha wino wa kuandika maneno yake".*

Kumkumbuka Allah kila wakati humuwezesha Muislamu kumuabudu Allah (s.w) katika maisha yake yote.



## Zoezi la Nne

1. Muislamu anatakiwa awe nadhifu wa

(a)..........................................................

(b)..........................................................

(c)..........................................................

(b)..........................................................

2. Faida tano za kupiga mswaki ni

(a)..........................................................

(b)..........................................................

(c)..........................................................

(b)..........................................................

(e)..........................................................

3. Muislamu huingia chooni kwa ......................na kusema..........................., kisha hutoka kwa............................akimshukuru Allah kwa kusema...............

4. Andika dua za matendo yafuatayo, kisha soma kwa sauti na kuzihifadhi

(a)kuvaa nguo mpya

(b)kupiga chafya

(c)kulala

(b)kutoka nyumbani

(e)kuanza kula na kumaliza



Book3.indb 76 4/19/05 7:05:50 AM

# Somo la 5. Tarekh

## UISLAMU WAKATI WA MTUME (S.A.W)

**Kipindi cha Makka**

Mtume Muhammad (s.a.w.) alipofikia umri wa miaka 40 alijiwa na Malaika Jibril alipokuwa katika pango la Jabal Hira. Malaika Jibril alimjia Mtume humo pangoni usiku wa manane katika kumi, la mwisho la mwezi wa Ramadhani. Jibril alimuamrisha Mtume kusoma. Mtume (s.a.w.) akamjibu kuwa hakuwa anaweza kusoma. Pamoja na jibu hili la ukweli, Jibril aliendelea kumlazimisha na kumbana Mtume mara tatu. Kisha mara ya nne Jibril alimsomea Mtume aya tano za kwanza za Surat-Alaq kama ifuatavyo:

ٱقۡرَأۡ بِٱسۡمِ رَبِّكَ ٱلَّذِي خَلَقَ ١ خَلَقَ ٱلۡإِنسَٰنَ مِنۡ عَلَقٍ ٢ ٱقۡرَأۡ وَرَبُّكَ
ٱلۡأَكۡرَمُ ٣ ٱلَّذِي عَلَّمَ بِٱلۡقَلَمِ ٤ عَلَّمَ ٱلۡإِنسَٰنَ مَا لَمۡ يَعۡلَمۡ ٥

*"Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba. Amemuumba mwanaadamu kwa A'laq. Soma na Mola wako ni karimu sana. Ambaye amemfundisha (mwanaadamu) kwa msaada wa kalamu. Amemfundisha mwanaadamu mambo aliyokuwa hayajui" (961-5).*

Baada ya kumsomea aya hizi malaika Jibril alijitambulisha kwa Muhammad na kumfahamisha rasmi kuwa yeye ni Mtume wa Allah (s.w.).

**Ujumbe wa Wahyi wa kwanza**

Tumejifunza kuwa wahay wa kwanza alioshushiwa Mtume (s.a. w.) ni hizo aya tano za mwanzo za Sural A'laq (96:1-5). Kutokana na aya hizi tunapata mafunzo yafuatayo:

- Kusoma au kutafuta elimu ndio amri ya kwanza kutoka kwa Mola wetu. Kabla Mtume (s.a.w.) hajapewa amri ya kusimamisha Swala, kutoa Zakat n.k. alipewa amri ya kusoma. Hii inaashiria kuwa iIi tuweze kuuhuisha Uislamu na kusimamisha Dola ya Kiislamu kama alivyosimamisha Mtume Muhammad (s.a.w.) ni lazima tuipe elimu kipaumbele.



Book3.indb 77 4/19/05 7:06:00 AM

- Waislamu tunaamrishwa tusome kwa ajili ya Allah (s.w.). Yaani tunaamrishwa tusome iIi tuweze kuishi Kiislamu katika maisha yetu yote. Tuweze kuongoza watu katika fani zote za maisha.

- Katika Uislamu hapana ubaguzi wa elimu. Hapana mgawanyiko wa elimu ya dini. na elimu ya dunia. Tumeamrishwa kujifunza fani zote za elimu ili tuweze kumjua Allah na kumwabudu. Tuweze kuwaonyesha walimwengu kwa vitendo ni ipi siasa bora, uchumi bora, utamaduni bora, amani na uhuru wa kweli. Ni Uislamu pekee unaoweza kuleta uhuru, haki na amani ya kweli hapa ulimwenguni.

- Chanzo cha fani zote za elimu ni Allah (s.w.). Hakuna elimu ambayo chanzo chake ni mwanadamu. Allah ndiye aliyemfunza mwanadau elimu zote. Wataalamu wote hugundua mambo kwa idhini yake.

**Ujumbe wa AI-Muzammil na AI-Muddaththir**
Wahay uliofuatia ni ule uliomo katika aya za mwanzo mwanzo za AI-Muzammil AI-Mudathir. Hebu tuanze kurejea aya surat Al-Muzammil:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡمُزَّمِّلُ ١ قُمِ ٱلَّيۡلَ إِلَّا قَلِيلٗا ٢ نِّصۡفَهُۥٓ أَوِ ٱنقُصۡ مِنۡهُ قَلِيلًا
٣ أَوۡ زِدۡ عَلَيۡهِ وَرَتِّلِ ٱلۡقُرۡءَانَ تَرۡتِيلًا ٤

*Ewe uliyejifunika maguo! Simama usiku (kucha kufanya Ibada); ila muda mdogo (tu hivi). Nusu yake au ipunguze kidogo. Au izidishe na soma Qur'an vilivyo (73:1-4)*

إِنَّا سَنُلۡقِي عَلَيۡكَ قَوۡلٗا ثَقِيلًا ٥ إِنَّ نَاشِئَةَ ٱلَّيۡلِ هِيَ أَشَدُّ وَطۡـٔٗا
وَأَقۡوَمُ قِيلًا ٦ إِنَّ لَكَ فِي ٱلنَّهَارِ سَبۡحٗا طَوِيلٗا ٧ وَٱذۡكُرِ ٱسۡمَ
رَبِّكَ وَتَبَتَّلۡ إِلَيۡهِ تَبۡتِيلٗا ٨

*Hakika sisi tutakuteremshia kauli nzito. Hakika kuamka usiku (na kufanya Ibada) kunawafikiana zaidi na moyo, na maneno (yake) yanatuwa zaidi.Hakika mchana una shughuli nyingi. Na litaje jina la Mola wako na ujitupe kwake kwa kweli (73:5-8)*


Book3.indb 78 4/19/05 7:06:21 AM

رَّبُّ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ فَٱتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٩﴾ وَٱصْبِرْ
عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَٱهْجُرْهُمْ هَجْرًا جَمِيلًا ﴿١٠﴾

*(Yeye ndiye) Mola wa mashariki na magharibi hakuna muabudiwa ila Yeye, basi mfanye kuwa mlinzi (wako). Na subiri juu ya haya wasemayo (hao makafiri) na uwaepuke mwepuko mwema.(73:9-10)*

Katika Wahy huu tunajifunza kuwa. Mtume (s.a.w) alipewa maandalizi maalumu yatakayo muwzesha kufanya kazi nzito ya kusimamisha Uislamu katika jamii: Maandalizi hayo ni:

(i) Kusimama usiku katika swala,

(ii) Kuisoma Qur'an vilivyo kwa mazingatio

(iii) Kumkumbuka Allah kila wakati kwa kuleta dhikiri mbalimbali

(iv) Kumtii Allah ipasavyo kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote

(v) Kujitegemeza kwa Allah na kumfanya Allah ndiye mlinzi pekee.

(vi) Kusubiri juu ya kero za Makafiri dhidi ya Uislamu.

Katika surat Al-Muddathir Mtume (s.a.w) aliongezewa ujumbe mwingine. Allah (s.w) alimwamrisha:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلْمُدَّثِّرُ ﴿١﴾ قُمْ فَأَنذِرْ ﴿٢﴾ وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ ﴿٣﴾

*Ewe uliyejifunika maguo! Simama usiku (kucha kufanya Ibada); Na Mola wako umtukuze. Na nguo zako uzisafishe.*

وَٱلرُّجْزَ فَٱهْجُرْ ﴿٥﴾ وَلَا تَمْنُن تَسْتَكْثِرُ ﴿٦﴾ وَلِرَبِّكَ فَٱصْبِرْ ﴿٧﴾



Book3.indb 79 4/19/05 7:06:39 AM

*Na mabaya yapuuze.Wala usiwafanyie ihsani viumbe ili upate kujikithirishia. Na kwa ajili ya Mola wako fanya subira.*

Katika aya hizi Mtume (s.a.w.) anazidi kuandaliwa na Mola wake kwa kuamrishwa afanye yafuatayo:

(i) Asimame kuufikisha ujumbe aliopewa na Mola wake.

(ii) Amtukuze Mola wake kila wakati

(iii) Awe msafi na twahara

(iv) Ayapuuze maneno mabaya kwa kujitenga mbali nayo

(v) Awafanyie watu lhsan kwa kutarajia kupata radhi za Allah (s.w.).

(vi) Afanye Subira kwa matarajio yakupata Malipo kwa Allah (s.w.).

Mtume (s.a.w.) na maswahaba zake waliyafuata vyema maelekezo hayo ya Mola wao. Hii ilimuwezesha Mtume na Maswahaba zake kusimamisha Dola ya Kiislamu kwa muda mfupi wa kipindi cha miaka 23 tu. Wakati wowote Waislamu wataweza kusimamisha Dola ya Kiislamu iwapo watamuiga Mtume katika kutekeleza maelekezo ya aya hizi.

**Kuanza kutangaza ujumbe**

Baada ya Mtume (s.a.w.) kupewa amri ya "Simama uonye" Alianza kazi yake kwa kumuendea mtu mmoja mmoja miongoni mwa watu wake wa nyumbani; rafiki zake na baadhi ya jamaa zake. Mkewe Khadija alikuwa wa kwanza kusilimu kisha wakafuatia Ally bin Abutalib na zaidi bin Harith. Wote hawa walikuwa katika familia ya Mtume (s.a.w.).

Abu Bakr (r.a.) rafiki yake Mtume (s.a.w.) alikuwa wa kwanza kusilimu katika watu wazima wenye hadhi katika mji wa Makka. Wengine waliosilimu mwanzoni mwa utume ni 'Uthman bin Affan, Zubair bin Awwam, 'Abdir-Rahman bin A'uf, Sa'd bin Abi-Waqqas, Talha bin U'baydillah, Arqam bin Abi Arqam na A'bdullah bin Mas'ud

Aliyoyasisitiza Mtume (s.a.w.) katika ujumbe wake wa mwanzo ni kuwataka watu washuhudie kwa dhati kuwa "Hapana Mola ila Allah na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah". Aliwaelekeza watu wamuabudu Allah (s..w.) peke yake na wasimshirikishe na chochote. Aliwataka watu wamuabudu Allah (s.a.w.) pekee kwa kutii maamrisho yake yote na kuacha, makatazo yake. Wamuombe yeye pekee na wamtegemee yeye pekee. Mtume (s.a.w.) aliwafundisha watu kuwa Wamtii na wamfanye kiigizo cha maisha yao. Alikuwa akijieleza kuwa yeye ni



Book3.indb 80 4/19/05 7:06:40 AM

Mtume wa Allah aliyekuwa akipata mwongozo kutoka kwake. Mtume (sa.w.) alitoa mafunzo hayo ya awali kwa kumuendea mtu mmoja mmoja kwa muda wa miaka mitatu ambapo watu wangi walisilimu.

**Kutangaza ujumbe kwa jamii mzima**

Baada ya miaka mitatu ya Utume, Muhammad (s.a.w.) alipewa amri na Mola wake kuufikisha ujumbe kwa watu wote.

وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ ٱلْأَقْرَبِينَ ٢١٤

*"Na uwaonye jamaa zako waliokaribu (Nawe)".(26:214)*

Mara tu baada ya kupokea amri hii Mtume (s.a.w.) alipanda juu ya kilima cha Sata na akanadi kuziita koo zote za kabila la Quraysh kila ukoo kwa jina lake. Baada ya koo zote kuhudhuria pale aliwaomba watu wasogee karibu yake kisha akaanza kutoa hutuba yake ya kwanza:

> *"Mnaonaje kama nikiwapa taarifa kuwa kuna jeshi kubwa linalokuja kukupigeni kutoka chini ya mlima huu. Je, Mtaniamini?" Wakajibu wote kwa pamoja, "Naam, bila shaka tutakuamini kwani hatujawahi kusikia kutoka kwako ila ukweli". Kisha Mtume (s.a.w.) alisema, "Hakika Mimi kwenu ni kama mtu aliyemuona adui, lakini akahofu kwamba adui anaweza kumuwahi kabla hajafikisha habari kwa watu wake, kwahiyo akaanza kupiga kelele, "tahadharini na mashambulizi ya asubuhi." Mtume (s.a.w.) akaendelea kuwaeleza, "Hakika mimi ni muonyaji kwenu juu ya adhabu kali iliyombele yenu. Enyi wana wa Abdul-Muttalib, "Enyi wana wa Abd al-Manaf, Enyi wana wa... mpaka akamaliza kuziita koo zote za Quraish "Hakika Allah ananiamrisha kuwaonya jamaa zangu wa karibu aliendelea Mtume (s.a.w.) kueleza. "Na hakika mimi sina cha kuwanufaisha katika maisha haya ya dunia na ya huko akhera ila mtakapokiri kuwa Hapana Mola ila Allah.*

Baada ya hutuba hii, wakuu wa kabila la Quraish walikasirika sana na wakasema kwa kelele, "umekuwa mwenda wazimu". Abu Lahab, ami yake Mtume, alimwapiza Mtume kwa kusema, "Iangamie mikono yako miwili siku ya leo. Hili ndilo ulilotuitia hapa?" Heshima yote tuliyokuwa tukikupa sasa umeikosa. Ondokeni mwacheni mpuuzi huyu".



Book3.indb 81 4/19/05 7:06:44 AM

Jambo hili lilimsononesha sana Mtume (s.a.w.), hasa ikizingatiwa kuwa Abu Lahaba alikuwa ami yake ilitarajiwa amsaidie Mtume, badala ya kuwa na kwanza kumvunja moyo katika kazi yake tukufu.

Allah (s.w) alimliwaza Mtume wake kwa kumshushia Sura iliyoyaelekeza maapizo yake kwa Abu Lahab mwenyewe.

تَبَّتْ يَدَآ أَبِى لَهَبٍ وَتَبَّ ﴿١﴾ مَآ أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُۥ وَمَا
كَسَبَ ﴿٢﴾ سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ﴿٣﴾

*Pana kuangamia mikono miwili ya Abu Lahab. Naye amekwisha angamia. Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma Atauingia moto wenye Muwako.*

وَٱمْرَأَتُهُۥ حَمَّالَةَ ٱلْحَطَبِ ﴿٤﴾ فِى جِيدِهَا حَبْلٌ
مِّن مَّسَدٍ ﴿٥﴾

*Na mkewe mchukuzi wa kuni (za fitina). Shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa."*

Mtume (s.a.w.) aliliwazika kwa aya hii na kuendelea na kazi yake ya kulingania Uislamu kwa watu wote aliannza na jamaa zake wa karibu. Watu waliouelewa ujumbe wa Uislamu kwa wepesi ni wote waliokuwa wanyonge miongoni mwa maskini, yatima na Watumwa. Waliona kuwa Uislamu ni dini ya kusimamisha haki katika jamii na kuondoa dhulma za aina zote.

Matajiri na wenye mamlaka na hadhi katika jamii waliupiga vita Uislamu kwa sababu ulizuia maslahi yao waliyokuwa wakiyapata kwa njia ya dhuluma. Mabwenyenye hawa walikuwa wakiwadhulumu maskini haki zao, wa kila mali za yatima na kuwafanyisha watumwa wao kazingumu na kuwatesa mateso ya kila aina. Hivyo walipoona kuwa kazi ya Uislamu ni kuondosha udhalimu huu na kusimamia kila mtu apate haki yake anayostahiki, walimchukia Mtume na Uislamu kuliko chochote kile.

**Upinzani dhidi ya Uislamu**

Mabwanyenye wa Makka, miongoni mwa matajiri na viongozi wa Kiqureishi, walikasirishwa sana na kitendo cha kusilimu watu wao hasa wote waliokuwa wanyonge wao. Walichukia sana kuenea kwa Uislamu kwa sababu kubwa zifuatazo:



Book3.indb 82 4/19/05 7:07:01 AM

(i) Maskini, Yatima, Watumwa na wanyonge wengine watakaposilimu watakosa watuwa kuwadhulumu.

(ii) Walihofia kuwa haohi zao zitashuka endapo wataheshimiwa na kutendewa sawa na maskini na watumwa. Katika Uislamu watu wote wanahadhi sawa mbele ya Allah (s.w.) na muheshimiwa zaidi mbele ya Allah (s.w.) ni yule amchaya zaidi.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَٰكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَٰكُمْ شُعُوبًا
وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓا۟ ۚ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ
عَلِيمٌ خَبِيرٌ ١٣

*Enyi watu! Kwa hakika Tumekuumbeni (nyote) kwa yule mwanaume(mmoja, Adam) na (yule yule) Mwanamke (mmoja, Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa(mbalimbali) ili mjuane (tu basi). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Allah zaidi katika nyinyi. Na Mwenyezi Mungu ni mjuzi mwenye habari(49:13).*

(iii) Baadhi ya koo zilihofia kupoteza nafasi yao ya Uongozi wa Makka endapo watamkubali Muhammad (s.a.w.) kuwa ni Mtume wa Allah (s.w.).

(iv) Wengine walihofia kuwa wakiacha ibada ya masanamu na kumwabudu Mungu mmoja tu, watapoteza haohi yao mbele ya Waarabu wote wa Bara Arab, waliopewa kutokana na utunzi na ulinzi wa Ka'abah. Ka'abah ilijazwa masanamu 360.

**Mateso dhidi ya Mtume na Waislamu katika kipindi cha Makka**

Wakuu wa Kiquraish walipoona Uislamu unazidi kuenea katika kona zote za Makka, walituma ujumbe na vitisho kwa Abu Talib, Ami yake na Mlezi wake Mtume (s.a.w.). Ujumbe huo ulikuwa na madhumuni ya kumkataza Mtume (s.a.w.) asiendelee kutangaza dini ya Allah kwa watu. Baada ya shinikizo kubwa kutoka kwa wakuu wa Kiquraish, ilibidi Abu Talib amkabili Muhammad (s.a.w.) na kumwambia, "Ewe mwana wa ndugu yangu, iokoe nafsi yangu na nafsi yako pia na usinitwishe mzigo nisiouweza, acha hii kazi yako (ya Utume). Kwa huzuni



Book3.indb 83 4/19/05 7:07:03 AM

kubwa, Mtume (s.a.w.) alimjibu Abu Taalib, "Ee mpendwa ami yangu, sitoiacha kazi hii hata kama wataliweka jua kwenye mkono wangu wa kulia na kuuweka mwezi kwenye mikono wangu wa kushoto. Ama Allah (s.w) atanipa ushindi au nitakufa katika kazi hii"

Baada ya ujumbe wao kukataliwa hivi Wakuu wa Kiquraishi walizidi kukasirika na kupitisha maazimio yafuatayo:

(i) Kufanya kila iwezekanavyo kuwazuia watu wasisilimu.

(ii) Kumpa adhabu kubwa kila anayesilimu

(iii) Aliyekuwa na haohi adharauliwe na asipewe tena ile heshima aliyokuwa akipewa hapo awali.

(iv) Kama ni mfanya biashara watu wasinunue kwake wala kumuuzia.

(v) Kama ni yatima asipewe mali yake.

Katika kutekeleza maazimio hayo makafiri wa Kiquraish walimtesa mtume na Waislamu mateso ya aina mbali mbali. Mtume mwenyewe alibughudhiwa kwa matusi na kejeli za namna kwa namna. Kwa mfano, walimwita Mtume, mwenda wazimu, mchawi, aliyepagawa na Shaitwaani, Abtar (aliyekatikiwa neema), mtunga mashairi, mwongo, na majina mengine mabaya, pia Maquraish wa Makka walimpiga Mtume na kufanya njama mbali mbali za kumuua.

Waislamu waliomuamini na kumfuata Mtume nao waliteswa sana na baadhi yao 'waliuliwa. Ifuatayo ni mifano michache ya mateso waliyopata baadhi ya Waislamu kwa kipindi hicho cha historia:

**(i) Abu Bakar (r.a.)**
Mara tu Mtume (s.a.w.) alipodhihirisha Utume wake hadharani, Abu Bakar alikwenda kwenye Ka'aba akatoa khutuba juu ya Uislamu. Watu wote waliokuwa pale walimvamia na kuanza kumpiga. Baada ya kuanguka chini, Utbah bin Rabi'ah alimpiga kwa viatu mpaka akazimia. Hakupata fahamu mpaka jamaa zake wakampeleka nyumbani kwake, na alikaa kitandani kwa masiku kutokana na kipigo hicho.

Mtume alipokuwa kwenye Ka'aba, Abu Jahl alikuja na kumtia shingoni kamba ya nguo iliyosokotwa. Aliinyonga ile kamba na kuikaza ili kumniga Mtume (s.a.w.) mpaka afe. Abu Bakar (r.a.) alipoona kitendo kile anafanyiwa Mtume



Book3.indb 84 4/19/05 7:07:03 AM

(s.a.w.), aliendа mara moja kumuokoa kwa kumsukumiza Abu Jahl pembeni na kuitoa ile kamba shingoni mwa Mtume (s.a.w.), kisha akasema: "Unataka kumuua mtu mzuri kama huyu ambaye ni Mtume wa Allah anayemtangaza Allah kwa sifa zake tukufu? Kisha Abu Jahl na maadui wengine wa Uislamu walimgeukia Abu Bakar na kumpiga kikatili.

**(ii) Bilal (r.a.)**

Bilal (r.a.) alikuwa Muhabesh na mtumwa wa Umayyah bin Khalaf,adui mkubwa wa Uislamu. Umayyah alikuwa akimpiga sana Bilal kisha alikuwa akimfunga kamba za mikononi, miguuni na shingoni na akiwaambia, watoto wamburure njiani. Mara nyingine alikuwa akimshindisha na kumlaza njaa, kisha siku ya pili yake alikuwa akimtoa nje na kumlaza chali uchi katika jua kali juu ya mchanga wa moto na kumuwekea jiwe kubwa la moto juu ya kifua chake na kumwambia: "Utasalia hivi hivi mpaka ufe au uache dini ya Muhammad. Bilal alikuwa akisema: "Ahad, Ahad-, yaani Naabudu Mungu mmoja tu. Alitaabishwa hivyo hivyo mpaka Abu Bakar '(r.a.) alipomkomboa. Abu Bakar (r.a.) aliwakomboa watumwa wengi waliokuwa wakiteswa kwa ajili ya Uislamu wao.

**(iii) Abu Fukayha (r.a.)**

Alikuwa akitaabishwa na kuteswa na mtoto wa Umayyah kwa namna ile ile alivyokuwa akitaabishwa Bilal.

**(iv) Bibi Zinira (r.a.)**

Abu Jahal alikuwa akikiunguza chuma motoni kisha akimgandamiza nacho machoni mpaka akapofuka.

**(v) Khabab (r.a.)**

Alikuwa mtumwa wa mwanamke katili kweli-kweli alikuwa akinyolewa nywele kisha akichomwa kwa bapa la chuma chenye moto juu ya kichwa. Akawa na madonda mengi kichwani.

**(vi) Ammar bin Yasir (r.a.)**

Baba yake na ndugu yake walikuwa wakipigwa kwa majani ya mitende kila siku mpaka wakajaa madonda mwili mzima. Baba yake na ndugu yake waliuli wa katika mateso hayo na akabakia Ammar (r.a.).

**(vii) Mama yake Ammar, bi Sumayya (r.a.)**

Pamoja na mateso mengi, aliuliwa kikatili mno. Alichomwa mkuki tumboni.

**(viii) Amir bin Fuhayra (r.a.)**

Aliadhibiwa kikatili mno mpaka akarukwa na akili.



Book3.indb 85 4/19/05 7:07:04 AM

**(ix) Bibi Lubayna (r.a.)**
Alikuwa akiadhibiwa kwa ukatili mno. Lubayna ni miongoni mwa wanawake mwanzo waliokubali kufuata mfumo wa maisha wa kiislamu wakati wa Mtume (s.a.w); kwa hakika aliukataa ujahili kwa gharama zote.

Hii ni mifano michache tu ya mateso dhidi ya Mtume na Waislamu. Takriban kila muislamu aliyesilimu katika kipindi cha Utume cha Makka aliteswa.

**Hijra ya Uhabeshia (Ethiopia)**

Mtume (s.a.w.) alipoona hali ya mateso kwa Waislamu imezidi kiasi cha kutoweza kuvumilika hasa kwa wote waliokuwa wanyonge, alitoa ruhusa kwa Waislamu kuhamia Uhabeshia (Ethiopia). Uhabeshia wakati huo ilikuwa ikitawaliwa na Dola ya Kikristo chini ya Mfalme Najash, aliyesifika kwa uadilifu.

Mnamo mwaka wa 615 A.D. msafara wa Waislamu wapatao 83 chini ya uongozi wa Jaffar bin. Abu Talib uliingia Uhabeshia na kupokelewa na mfalme Najash. Msafara huu ulifuatiliwa na Maquraish kwa nia ya kuwarudisha- Makka iIi waendelee kupata mateso na kuzuia Uislamu usije enea huko Uhabesh. Walimtuma Amr bin AI-'As na mwenzie, 'Abdullah bin Abi Rabi'ah wende Uhabesh kuwarudisha Waislamu Makka. Wajumbe wa Maquraish walipofika kwa mfalme walidai kuwa wanawaomba Waislamu warudi nao Makka wakaadhibiwe kwa kosa la kuiacha dini ya Mababu zao na kufuata dini mpya ambayo iliwagawa watu wao na kuleta mtafaruku mkubwa katika jamii.

Mfalme muadilifu, kabla ya kutoa uamuzi ilibidi awafikishe wote mbele ya Mahakama yake iIi apate kusikiliza pande zote mbili. Mfalme aliwaelekea Waislamu na kuwauliza, "Dini yenu hii ni dini gani ambayo imewagawa watu wenu na ambapo hamjajiunga na dini yangu ya Ukristo au dini yoyote ile iliyojulikana?"Alijibu Jaffar (r.a;) kwa niaba ya Waislamu wenzake:

> **"Ewe mfalme, sisi tulikuwa waovu na majahili, tuliabudu masanamu na kula nyamafu, hata mizoga ya wanyama waliokufa wenyewe. Tulifanya kila aina ya matendo machafu na ya aibu, hatukuwa wenye kuwajibika kwa jirani na jamaa zetu. Wenye nguvu miongoni mwetu waliwakandamiza wanyonge. Kisha Allah (s.w.) akamleta mtume miongoni mwetu ambaye tulimfahamu vema kwa nasaba yake, utukufu wake na uzuri wa tabia yake tukufu. Alituita tumuabudu Mungu mmoja tu na akatukataza kuabudia masanamu na mawe. Alitufundisha kusema ukweli, kutunza amana, kuwaangalia ndugu na jamaa na kuvvafanyia wema. Alituamrisha kusimamisha swala na**


Book3.indb 86 4/19/05 7:07:04 AM

**kutoa zakat. Alituamrisha kujiepusha na maovu na kujiepusha na umwagaji damu. Alitukataza zinaa, kusema uwongo, kula mali ya Yatima na kuwasingizia uovu wanawake wataharifu. Alitufundisha Qur-an. Tulipomuamini na kuishi kulingana na mafundisho yake mazuri, watu wetu walianza kutupiga na kututesa wakidhania kuwa tutaiacha dini yetu na kurudia ibada ya masanamu. Ukatili wao dhidi yetu ulipokithiri ndipo tukaja kujihami katika nchi yako kwa ruhusa ya Mtume wetu".**

Kisha Mfalme Najash alimtaka Jaffar amsomee habari za Nabii Isa (a.s.) katika Qur-an. Alimsomea aya za Surat Mariam, zinazoelezea juu ya kuzaliwa kwa muujiza kwa Nabii Isa (a.s.). Kisomo cha Qur'an kilimgusa sana mfalme ambaye alikiri. "Naapa kwa jina la Allah kuwa maneno hayo na yale ya Biblia ni mionzi ya mwanga inayotoka katika chanzo kimoja".

Baada ya maelezo hayo ya Waislamu mfalme aliwaruhusu kuishi kwa amani katika nchi yake na kuyakatalia mbali madai ya wajumbe wa Makafiri wa Kiquraish.

**Waislamu watengwa**

Makafiri wa Kiquraish walikasirika sana waliposhindwa kuwarejesha Waislamu waliohamia Uhabesh. Waliutaka ukoo wa Banu Hashim ukubali kumtoa Muhammad (s.a.w.) auawe na badala yake wapewe 'Umarah bin Walid al-Mughira. Abu Twalib kwa niaba ya Banu Hashim wote isipokuwa Abu Lahab. alikataa ombi liIe. Wakuu wa Kiquraish walizidi kukasirika. Walipitisha uamuzi wa kuwasusa (kuwatenga) Waislamu wote. Walibandika mkataba wasusie ndani ya Ka'aba kuwa Mqurash yeyote haruhusiwi:

(i) Kusema na Banu Hashimu yeyote awe Muislamu au asiwe Muislamu."

(ii) Kuwauzia Banu Hashim chochote wala kununua chochote kutoka kwao.

(iii) Kuoana na Banu Hashim.

(iv) Kuwasaidia Banu Hashim kwa namna yoyote ile.

(v) Kukaa pamoja na Banu Hashim.

Baada ya tangazo hili Waislamu'na Banu Hashimu walifukuzwa mjini Makka na nyumba zao pamoja na vitu vyao kuchomwa moto na kuharibiwa.



Book3.indb 87 4/19/05 7:07:05 AM



Walihamia kwenye bonde moja nje ya mji wa Makka ambalo lilijulikana kwa jina la Shi'b Abu Talib yaani makazi ya Abu Talib. Maisha yao katika bonde hili yalikuwa magumu sana. Paliwekwa ulinzi mkali wa kuzuia watu wenye huruma. wasiwaletee chakula au huduma yoyote ile. Makazi yao yalikuwa duni sana. Walipigwa na jua kali jangwani wakati wa mchana na baridi kali nyakati za usiku. Walikosa chakula mpaka ikabidi wale majani na ngozi. Walidumu katika mateso hayo kwa muda wa miaka mitatu. Afya zao ziliathirika sana na kuwa sababu ya kifo cha mkewe Mtume Bibi Khadija, na Abu Talib. Mkataba wa Susio ulivunjwa na baadhi ya wakuu wa Kiquraishi baada ya kushindwa kuvumilia kuwaweka wenzao katika mateso kiasi kile. Walikuwemo watoto wachanga na vikongwe katika mateso hayo.

**Mtume (s.a.w) kwenda Taif kulingania Uislamu**

Baada tu ya kurejea Makka kutoka Shi'b Abu Talib, Abu Talib alishikwa na ugonjwa na kufariki mnamo 620 A.D. akiwa na umri wa miaka 82. Baada ya siku tatu alifariki Bibi Khadija akiwa na umri wa miaka 65. Bibi Khadija na Abu Talib walitoa mchango mkubwa katika kuuhami Uislamu na Waislamu. Hivyo ilikuwa msiba mkubwa sana kwa Mtume (s.a.w.) na Waislamu kuondokewa na watu hawa. Mtume (s.a.w.) aliuita mwaka ule "Mwaka wa Huzuni". Ulikuwa mwaka wa kumi baada ya kupewa utume.

Baada ya kumaliza msiba, Mtume (s.a.w.) aliamua kwenda kulingania Uislamu katika mji wa Taif akiwa ameandamana na Zaidi bin Harith, mtoto wake wa kulea. Talf ni mji aliokuwa akiishi Bibi Halima mama yake Mtume wa kunyonya. Kwa mahusiano haya alikuwa na matumaini makubwa kuwa watu



Book3.indb 88 4/19/05 7:07:06 AM

wa mji huu watasikiliza na kuufuata ujumbe wake. Mambo yalitokea kinyume chake. Walikataa kabisa kumsikiliza. Walipoona kuwa mtume anaendelea tu bila ya kukata tamaa, wakazi wa mji huu waliwaamuru watoto wamkimbize kwa mawe. Waliwakimbiza na kuwapopoa kwa mawe mpaka Mtume na Zaid wakavuja damu mwili mzime.

Pamoja na kufanyiwa ubaya kiasi hicho na wakazi wa Taif Mtume (s.a.w.) hakuthubutu kuwalaani watu hao wala hakutaka watu hao waangamizwe. Bali alimjibu Malaika aliyekuwa tayari kuwaangamiza watu hao kwa amri ya Mtume kutokana na idhini ya Allah (s.w.):

> *"Hata kama watu hawa hawaukubali Uislamu, ninategemea kwa Allah kuwa watatokea watu katika kizazi hiki watakaomuabudu Allah (s.w.) na kupigania dini yake."*

**Mafunzo kutokana na mateso yaliyompata Mtume na Waislamu**
Kutokana na mateso aliyopata Mtume (s.a.w.) na Waislamu kwa ajili ya kusimamisha Uislamu katika jamii tunajifunza kuwa:

(i) Uislamu ni dini yenye maadui wengi. Maadui wake wakubwa ni Wakuu wa jamii za kikafiri miongoni mwa matajiri na Watawala. Hofu ya wakuu ni kuwa Wakiuachia uislamu ukasimama watakosa maslahi yao ambayo huyapata kwa njia ya kuwadhulumu wanyonge. Uislamu ni dini ya kuwatetea wanyonge na kuwazuia Madhalimu wasidhulumu.

(ii) Makafiri hawana uwezo wa kuzuia dini ya Allah isisimame pale watakapo jitokeza Waislamu kuisimamisha. Allah (s.w.) analiweka hili bayana katika aya zifuatazo:

يُرِيدُونَ لِيُطْفِـُٔوا۟ نُورَ ٱللَّهِ بِأَفْوَٰهِهِمْ وَٱللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِۦ وَلَوْ كَرِهَ
ٱلْكَٰفِرُونَ ﴿٨﴾ هُوَ ٱلَّذِىٓ أَرْسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلْهُدَىٰ وَدِينِ ٱلْحَقِّ
لِيُظْهِرَهُۥ عَلَى ٱلدِّينِ كُلِّهِۦ وَلَوْ كَرِهَ ٱلْمُشْرِكُونَ ﴿٩﴾

> *"Wanataka kuzima nuru ya Allah (Uislamu) kwa vinywa vyao, Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri watachukia. Yeye (Allah) ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na kwa Dini ya haki iIi kuifanya ishinde dini zote ijapokuwa washirikina watachukia.(61:8-9)"*



Book3.indb 89 4/19/05 7:07:18 AM

(iii) Muumini wa kweli ni yule aliyetayari kusubiri na kukabiliana na hali yoyote ngumu iwayo kwa ajili ya kusimamisha Uislamu. Muumini wa kweli ni lazima afikwe na misukosuko kwa ajili ya Uislamu. Allah (s.w.) anatukumbusha katika aya zifuatazo:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا۟ ٱلْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُم مَّثَلُ
ٱلَّذِينَ خَلَوْا۟ مِن قَبْلِكُم ۖ مَّسَّتْهُمُ ٱلْبَأْسَآءُ وَٱلضَّرَّآءُ
وَزُلْزِلُوا۟ حَتَّىٰ يَقُولَ ٱلرَّسُولُ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مَعَهُۥ مَتَىٰ
نَصْرُ ٱللَّهِ ۗ أَلَآ إِنَّ نَصْرَ ٱللَّهِ قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾

*Mnadhani kuwa mtaingia peponi na hali hamjajiwa na mfano wa (yale yafiyowajia) wale waliopita kabla yenu? Yaliwapata mashaka na madhara na wakatetemeshwa sana hata mitume na walioamini pamoja nao wakasema, Nusura ya Mwenyezi Mungu itafika lini?" Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu iko karibu," (2:214)*

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا۟ ٱلْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ
جَٰهَدُوا۟ مِنكُمْ وَيَعْلَمَ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٤٢﴾

*Jel Mnadhani mtaingia peponi hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wote waliopigania dini ya Mwenyezi Mungu miongoni mwenu na kuwapambanua waliofanya subira?" (2:142)*

### Safari ya Miiraji

Katika mwaka wa 12 baada ya kupewa utume sawa na mwaka 621 A.D. Mtume (s.a.w.) alichukuliwa usiku na Malaika Jibril kwa safari ndefu sana lakini iliyochukuwa muda mfupi sana. Safari hii iligawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni Safari ya hapa Ardhini kutoka Msikiti Mtukufu wa Makka, Ka'aba mpaka msikiti Mtukufu wa Aqswaa (Baitul-Maqdis) ulioko Jerusalem.




Book3.indb 90 4/19/05 7:07:40 AM

Safari hii ya Ardhini inajulikana kwa jina la "Israa" kama ilivyotajwa katika Qur'an:

سُبْحَٰنَ ٱلَّذِىٓ أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِۦ لَيْلًا مِّنَ ٱلْمَسْجِدِ
ٱلْحَرَامِ إِلَى ٱلْمَسْجِدِ ٱلْأَقْصَا ٱلَّذِى بَٰرَكْنَا حَوْلَهُۥ
لِنُرِيَهُۥ مِنْ ءَايَٰتِنَآ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ ١

*"Utukufu ni wake Yeye ambaye alimpeleka mja wake usiku kutoka msikiti mtukufu (wa Makka) mpaka msikiti wa Mbali (Masjidiul Aq-swaa) ambao (tumeubariki na) tumevibariki vilivyomo pembezoni mwake, iIi tumuonyeshe baadhi ya alama zetu. Hakika yeye Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, mwenye kuona." (17:1).*






Book3.indb 91 4/19/05 7:07:52 AM



Sehemu ya pili ilikuwa ni safari ya kwenda mbinguni kutoka pale Masjidul Aqswaa mpaka mbingu ya Saba. Safari hii inajulikana kwa jina la Miiraji. Sehemu hii ya pili imeelezwa katika Qur'an kama ifuatavyo:

أَفَتُمَٰرُونَهُۥ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ ﴿١٢﴾ وَلَقَدْ رَءَاهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ ﴿١٣﴾
عِندَ سِدْرَةِ ٱلْمُنتَهَىٰ ﴿١٤﴾ عِندَهَا جَنَّةُ ٱلْمَأْوَىٰٓ ﴿١٥﴾
إِذْ يَغْشَى ٱلسِّدْرَةَ مَا يَغْشَىٰ ﴿١٦﴾

*"Na (Mtume) akamuona (Jibril) mara nyingine (kwa sura yake ya kimalaika katika usiku wa Miiraji). Penye mkunazi wa kumalizikia mambo yote. Karibu yake ndio kuna hiyo Bustani (Pepo) itakayokaliwa (na Watu wema). Kilipoufunika Mkunazi hiyo kilichoufunika.*

مَا زَاغَ ٱلْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ ﴿١٧﴾ لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ ءَايَٰتِ رَبِّهِ
ٱلْكُبْرَىٰٓ ﴿١٨﴾

*Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka (uliowekewa). Kwa yakini aliona (Nabii Muhammad) mambo makubwa kabisa katika alama za Mola wake. (53: 13-18).*

Lengo kubwa la Safari ya Israa na Miiraji ni kumyakinisha Mtume zaidi katika kazi yake. Akiwa Mtume na kiongozi wa Ulimwengu mzima alitakiwa awe na ujuzi na uzoefu wa ziada kuliko walimwengu wote na mitume wote walio mtangulia. Hivyo Allah (s.w.) alimwandalia safari hii ili amuonyeshe baadhi ya alama zake, kama anavyosisitiza:

لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ ءَايَٰتِ رَبِّهِ ٱلْكُبْرَىٰٓ ﴿١٨﴾

*"Kwa yakini aliona mambo makubwa katika alama za Mola wake." (53:18)*

**Mikataba ya Aqaba**

Mtume (s.a.w.) alitumia kila fursa aliyoipata katika kutangaza Dini ya Allah (s.w). Wakati wa Hija walikuja watu kutoka kona zote za Bara Arab na nje ya Bara Arab. Wakuu wa makafiri wa Kiquraishi walikuwa wakiwaweka watu wao katika kila njia inayoingia Makka ili kuwatahadharisha Wageni mafundisho ya Uislamu to kwa Muhammad. Pamoja na harakati hizi za Makafiri za kuzuia Dini ya Allah isiwafikie watu, bado Mtume (s.a.w.) alifanikiwa kuwapata wageni na kuwafikishia ujumbe wa Uislamu. Katika wageni aliokutana nao wakaupokea ujumbe wa Uislamu kwa wepesi ni Watu wa Yathrib (Madina). Katika mwaka wa 20 A.D. watu sita kutoka Yathrib, katika kabila la Khazraj walikutana na Mtume katika Jamaratul-Aqaba huko Mina karibu na mji wa Makka. Watu hawa walisilimu baada ya kupata ujumbe wa Mtume na kuahidi kufikisha ujumbe wa Uislamu huko kwao.

Katika Hija iliyofuatia, 621 A.D.; Mtume alikutana na Waislamu 12 kutoka Yathrib, 10 kutoka kabila la Khazraji na wawili kutoka kabila la Aus. Aus na Khazraji ni makabila makubwa ya Waarabu wa Yathrib ambayo yalikuwa maadui wao kwa wao kabla ya Uislamu kuingia humo. Baada ya Mtume kuwapa mafundisho ya Uislamu, waliomba Mtume ampeleke mwalimu atakayafundisha Uislamu na kuutangaza huko Yathrib. Mtume (s.a.w.) aliwakubalia na akampeleka Mus'ab bin Umair pamoja nao.

Hija iliyofuatia, 622 A.D., Walimjia Mtume Waislamu 75 kutoka Yathrib, wawili wakiwa wanawake. Mtume (s.a.w.) aliongozana na AbuBakr (r.a.) Aly bin Abu Talib (r.a.) na Abbas bin Abdil-Mutalib. Walikutana kwa siri na hawa Waislamu wa Yathrib karibu na Jamaratul Aqabah. Baada ya kuwapa mawaidha juu ya Uislamu, Mtume (s.a.w.) aliwataka watoe ahadi kuwa watawahifadhi Waislamu endapo watahamia kwao. Waislamu hao walitoa ahadi kuwa watamhifadhi Mtume na Waislamu watakaohama naye kwa nafsi na mali zao. Makubaliano hayo hujulikana kama **mkataba wa Aqabah**.



Book3.indb 93 4/19/05 7:08:11 AM

**Waislamu kuhamia Yathrib**

Baada ya wale Waislamu 75 kurejea salama Yathrib Mtume (s.a.w.) aliwaita Waislamu na kuwapa habari njema kwa kusema, "Allah (s.a.w.) keshakupeni mahali pazuri pa amani pa kukaa na kuendeleza dini yenu bila ya kuteswa na yeyote. Mahali penyewe ni **Yathrib**. Nimekwishapata habari kuwa ndugu zenu wako tayari kukupokeeni kwa hali na mali. Basi kila aliyetayari aondoke leo asingoje kesho. Baada ya ujumbe huu Waislamu walianza kuhama kwa siri siri kwenda Yathrib.



**Mtume(s.a.w) kuhamia Yathrib**

Makafiri wa Kiquraish walikasirishwa sana na kitendo cha Waislamu kuhamia Yathrib. Isitoshe walishakuwa na wasi wasi kuwa huenda Mtume naye atahama kisiri siri na kuupa nguvu Uislamu. Kwa hiyo wakuu wa Kiquraish katika Darul Nadwa (ukumbi wa Bunge lao) wakapanga njama za kumuua.

Walikubaliana kwa pamoja kuwa wachaguliwe vijana kutoka kila ukoo wa kabila la Qur'aish, isipokuwa Bani Hashim, kisha kila mmoja apewe upanga mkali. Waizingire nyumba ya Mtume usiku na wamuue wote kwa pamoja wakati wa alfajiri.


Allah (s.w.) alimfahamisha Mtume wake juu ya njama hiyo na kumuamuru aondoke usiku huo huo waliopanga kutekeleza njama yao. Baada ya amri hii Mtume (s.a.w.) akishirikiana na Sahib yake, Abu Bakr, walipanga uzuri utaratibu wa safari yao ya kweda Yathrib. Walipanga kuwa watajificha, kwenye pango la **Thaur** kwa siku tatu na waliweka utaratibu wa kupata chakula na habari za makafiri wa Makka. Pia walimkodi mtu aliyewaongoza kwenda Yathrib kwa kupitia njia za siri. Mambo yote yalikwenda kama yalivyopangwa.

Usiku waliokusudiwa kuuawa Mtume ulipofika, Mtume (s.a.w.) alianza safari yake akiongozana na Abu Bakr (r.a.). Aliwaacha wote wauaji nje ya nyumba



Book3.indb 94 4/19/05 7:08:12 AM

yake wakiwa wamelala fofofo. Asubuhi walipogundua kuwa Mtume na Abu Bakar hawapo, Wakuu wa Makka walikasirika sana na wakatangaza zawadi nono ya ngamia 100 kwa yeyote atakayamleta Muhammad akiwa hai au akiwa amekufa. Walihangaika sana kumtafuta lakini hawakumuona. Walifika karibu sana na lile pango la Thaur, lakini Allah (s.w.) aliwahifadhi waja wake wasiweze kuonekana.



Utando wa Buibui katika lango uliwakatisha tamaa kuwa haiwezekani Mtume na Abubakar kuingia mle alfajiri ile. Hivi ndivyo Allah alivyo mnusuru Mtume na Sahib yake kama tunavyojifunza katika Our-an:

إِلَّا تَنصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ ٱللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ
ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ ثَانِىَ ٱثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِى
ٱلْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَٰحِبِهِۦ لَا تَحْزَنْ إِنَّ
ٱللَّهَ مَعَنَا ۖ فَأَنزَلَ ٱللَّهُ سَكِينَتَهُۥ عَلَيْهِ
وَأَيَّدَهُۥ بِجُنُودٍ لَّمْ تَرَوْهَا

*Kama hamtamnusuru Mtume, basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wole waliokufuru alipokuwa (mmoja tu na mwenziwe) wa pili yake.Walipokuwa wote wawili katika pango, (Mtume) alipomwambia Sahib yake usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi. Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona..." (9:40).*

Baada ya siku tatu ndani ya pango, msafara wa Mtume ulielekea Yathrib na kufika huko salama salmini. Kwa heshima ya Mtume, mji wa Yathrib ulibadilishwa jina na kuitwa Madinatun-Nabii (mji wa Mtume) na AI-Madinal al-Munawwar.



Book3.indb 95 4/19/05 7:08:30 AM



## Zoezi la Tano

1. Muhammad alipewa Utume akiwa na miaka................ usiku wa ............. katika pango la..................................

2. Ujumbe wa kwanza ambao malaika alimsomea Mtume ulihusu..... .....................................

3. Taja mafundisho kumi aliyofunzwa Mtume (s.a.w) ili aweze kulingania watu Dini ya Uislamu.

4. Taja wanawake waumini watatu waliosilimu mwanzoni

5. Waliokuwa mstari wa mbele kumpinga Mtume (s.a.w) walikuwa.. ............................. na ..................................

6. Taja matendo waliyofanya makafiri wa Makka katika kuwapiga vita Waislamu

7. Waislamu walipohamia Habash, makafiri walifanya nini?

8. Mwaka wa huzuni ni ule alimofariki..................... na .................. ambapo Allah alimliwaza na kumtia nguvu Mtume (s.a.w) kwa safari ya ............................... na ................................

9. Waislamu walihamia Yathrib baada ya Mtume (s.a.w) kufunga ................ miwili ya ......................... na waislamu kabila la ................ na .......................

10. Wakuu wa makafiri walikutana ................................ wakajadili mambo matatu ya kumfanya Mtume (s.a.w) ambayo ni................... ..., au ................................ ama .................................



Book3.indb 96 4/19/05 7:08:30 AM